




Madereva bodaboda bajaji waandamana kupinga zuio mjini

UKURASA 3





# Nipashe

Ijumaa Aprili 22, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580923

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Sakata jiwe madini rubi latikisa Bunge



• Ni la thamani ya bil. 240/- kutoka Tanzania, latangazwa mnadani Dubai, serikali yatoa kauli... *Uk. 2*



Mapadri wa Kanisa Katoliki, wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Paroko wa Parokia ya Mbezi Mshikamano, Padre Francis Kangwa, baada ya kuwasili katika Kituo cha Hija cha Pugu, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya misa na maziko. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Askofu Ruwa'ichi na familia wanena maziko ya padri aliyefariki Dar

UKURASA 3

## YALIYOMO

### CAG ABAINI MABILIONI YAKO HATARINI KUPOTEA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini mabilioni ya shilingi yako hatarini kupotea kutokana na kutokuwa na udhibiti mzuri wa usimamizi wa mikopo inayotolewa na halmashauri kwa makundi maalum.

UKURASA 4

### WABUNGE WAIBANA SERIKALI KUTOA AJIRA

SERIKALI imesema katika mwaka wa fedha 2022/23 itaajiri watumishi wapya 30,000 katika kada mbalimbali zikiwamo za afya na elimu watakaoigharimu zaidi ya Sh. bilioni 120.

UKURASA 4

### MSHANGAO MELI ZA NYASA MAKABIDHIANO KUFANYIKA MWANZA

KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida, mchakato wa makabidhiano ya meli za Ziwa Nyasa kutoka Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kwenda kwa Kampuni ya Meli Tanzania (MSCL), umeanza kufanyikia mkoani Mwanza badala ya Mbeya mahali zilipo meli hizo.

UKURASA 16

# Utata watanda madai ya kukamatwa wakili maarufu

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA YAIMARISHA ULINZI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Sakata jiwe la rubi latikisa Bunge

**Na Augusta Njonji,** DODOMA

MJADALA umeibuka bungeni na mitandao ya kijamii baada ya jiwe lenye madini aina ya rubi lenye uzito wa kilo 2.8 kuonekana katika maonyesho jijini Dubai, huku likidaiwa limetoka Tanzania.

Jiwe hilo lenye thamani ya Dola za Marekani milioni 120 (Sh. bilioni 240) limeibua gumzo baada ya kutofahamika limepita njia gani hadui kufika Dubai, huku serikali ikikiri kupata taarifa za uwapo wa jiwe hilo, kuanza kukusanya taarifa za kiuchunguzi na kuahidi kuzitolea ufafanuzi bungeni.

Akitoa ufafanuzi bungeni jana, Naibu Waziri wa Madini, Dk. Stephen Kiruswa, wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mkinga (CCM), Dunstan Kitandula, alisema taarifa za awali zinaonesha kuwa mmiliki wa sasa wa jiwe hilo anaishi Marekani katika Jimbo la California na tayari serikali imeanza kuwasiliana naye tangu juzi.

Katika swali lake, Kitandula aliuliza: "Jiwe la rubi lenye uzito wa kilo 2.8 lipo kwenye maonyesho kwa sasa jijini Dubai na linasadikika kutoka Tanzania na siku chache zijazo kutakuwa na mnada wa kuuza jiwe hilo. Je, nchi itanufaika vipi na mnada huo?"

Akijibu swali hilo, Dk. Kiruswa alisema Aprili 13, mwaka huu, Wizara ya Madini ilipata taarifa kupitia mitandao ya kijamii kwamba kuna jiwe ambalo limepewa jina Akbar Alhamal ambalo linakwenda kuwekwa mnadani ndani ya siku 30 baada ya mfungo wa Ramadhan na kudaiwa limetoka Tanzania.

"Mheshimiwa Spika, mara baada ya kupata habari hizo, wizara imechukua hatua za haraka kutafuta kama habari hizo ni za kweli. Kwa kuwa jiwe limeshavuka mipaka ya Tanzania, tunaendelea kukusanya taarifa ili kuzitoa katika bunge lako tukufu, zinahusisha nchi ya Dubai na tayari ubalozi wa Tanzania na wizara zinawasiliana kufuatilia ukweli na uhalisia wa bei,"alisema.

Dk. Kiruswa alisema kutokana na mmiliki wa sasa wa jiwe hilo kuwa yuko Marekani, wigo wa kidiplomasia umepanuka kutokana na kuhusisha nchi tatu.

"Nikuhakikishie Mheshimiwa Spika kwamba tutakapokuwa tumepata nyaraka za usafirishaji wa jiwe hili kama kweli limetoka Tanzania, tutapata nyaraka za thamani na asili ya hili jiwe limetoka wapi, tukipata na nyaraka za mauziano za mmiliki wa sasa na wa awali, tutatoa taarifa katika bunge lako kama lipo na kama ni la kwetu, tuwahakikishie Watanzania haki yao haitapotea na sheria, kanuni na taratibu zitahakikisha rasilimali hii inatumika kwa manufaa ya nchi yetu," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Rorya (CCM), Jafari Chege, alihoji ni lini uchimbaji wa madini ya dhahabu utaanza katika eneo la Utegi katika Tarafa ya Girango.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema Wizara ya Madini imeendelea kutoa leseni za utafutaji wa Madini nchini.

"Katika eneo la Utegi kuna leseni za utafutaji wa madini za Kampuni ya North Mara Gold Mine Limited na ABG Exploration Limited. Kwa sasa kampuni hizi zinaendelea na utafutaji wa madini katika eneo hilo," alisema. Pia alisema uchimbaji wa madini hutegemea kukamilika kwa mafanikio kwa utafutaji wa madini ambao huhusisha shughuli za kijiolojia.

"Aidha, shughuli hizi huchukua gharama kubwa na muda mrefu. Kwa msingi huo, eneo la Utegi linatarajiwa kuanza uchimbaji baada ya utafiti kukamilika na kuonekana kwa mashapo yenye kutosheleza kuanzisha uchimbaji kwa faida,"alisema.

Pia alisema serikali kupitia Tume ya Madini inafuatilia kwa karibu shughuli za utafutaji wa madini zinazofanyika nchi nzima.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akiwa katika mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi, Ofisini kwake Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Adaiwa kumpa dawa mwanamke, kumbaka

**Na Kulwa Mzee**

MKAZI wa jijini Dar es Salaam, Borgias Kwitega, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za kumwekea dawa za kupumbaza mwanamke, kumbaka na kuiba simu.

Kwitega na mshtakiwa Abdallah Mmanyi ambaye anakabiliwa na shtaka la kupokea mali ya wizi, wamefikishwa jana mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ramadhani Rugemarila na kusomewa mashtaka na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Lucy Uisso.

Mshtakiwa wa pili Ally Kibuga, hakufikishwa mahakamani hapo, kwa kile kilichoelezwa kuwa bado yupo mikononi mwa polisi.

Wakili Uisso alidai washtakiwa kwa pamoja wanakabiliwa na kesi ya jinai namba 64/2022 na katika shtaka la kwanza, Kwitega anadaiwa kumwekea vidonge vya kupumbaza mwanamke.

Inadaiwa tukio hilo alitenda Januari 24, 2022 eneo la Rumix Hotel iliyopo Kinondoni, alimpa vidonge vya kupumbaza, mwanamke mwenye umri wa miaka 30.

Shtaka la pili, siku na eneo hilo, Kwitega alimbaka mwanamke huyo, bila ridhaa yake.

Shtaka la tatu, Kwitega anadaiwa kuiba simu aina ya iPhone yenye thamani ya Shilingi milioni tatu pamoja na nguo zenye thamani ya Sh. 300,000, vyote vikiwa na thamani ya Sh milioni 3.3.

Shtaka la nne ni kupokea mali ya wizi tukio, linalowakabili mshtakiwa Kibuga na Mmanyi.

Wakili Uisso, alidai washtakiwa hao wanadaiwa katika tarehe tofauti mwaka 2022, walipokea simu aina ya iPhone huku wakijua kuwa mali hiyo ni ya wizi.

Upande wa mashtaka ulidai kuwa upelelezi wa shauri hilo umekamilika na wanaomba tarehe nyingine.

Hakimu Rugemarila alitaja masharti ya dhamana kuwa kila mshtakiwa anatakiwa kusaini hati ya dhamana ya Shilingi milioni mbili.

Pia, washtakiwa hao wanatakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye barua za utambulisho kutoka Serikali ya Mitaa.

Hata hivyo, washtakiwa hao wameshindwa kutimiza masharti ya dhamana na kurudishwa rumande.

# Utata waibuka madai ya kukamatwa wakili maarufu

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya taarifa kuhusu kutoweka kwa wakili na mwanaharakati Peter Madeleka, utata ulitanda kwenye mitandao ya kijamii huku chama cha ACT-Wazalendo kikieneza ujumbe wa hashtag#FreeMadeleka.

Katika ukurasa wa mtu anayetambulika kwenye mtandao wa kijamii tweeter, Hilda Newton, ilielezwa kuwa: "Familia ya Madeleka wamefika Central Police (Kituo Kikuu cha Polisi) Dar muda huu kwa ajili ya kujua Madeleka kakamatwa kwa kosa gani lakini wameambiwa kwamba jeshi la polisi hawajamkamata wala hawamshikilii Madeleka."

Msemaji wa ACT Wazalendo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mbarala Maharagande, kwenye ukurasa wake wa tweeter jana aliandika: "Jeshi la Polisi limtendee haki kwa mujibu wa Sheria Wakili Peter Madeleka kutokana na kumkamata kinyume cha taratibu na kutoruhusu ndugu wala wanasheria wake kuonana naye."

Aidha Nipashe ilipomtafuta Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, Jumanne Muliro, iwapo wanamshiilia wakili huyo, alisema: "Hapana, hatumshikilii. Kwa taarifa zaidi atafutwe kamanda wa mkoa wa Arusha".

Kwenye ukurasa wa tweeter wa chama hicho ilielezwa zaidi kuwa tukio hilo lilitokea juzi katika Hoteli ya Serena kwa watu wanaosadikiwa ni maofisa wa polisi wasio na utambulisho wowote na gari lisilo na namba za usajili wa polisi, walifika hotelini hapo na kumchukua wakili huyo bila kufuata taratibu za kisheria.

"Baadaye, baada ya ndugu na jamaa wa karibu kufuatilia, ndipo polisi walikiri kumshikilia. Siku za hivi karibuni, Wakili Peter Madeleka amekuwa akiishinikiza serikali kuwachukulia hatua maofisa wa Idara ya Uhamiaji waliofanya ubadhirifu wa utengenezaji wa stika feki za VISA kama ambavyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), alivyobainisha kwenye taarifa yake ya ukaguzi wa 2020/2021," ilisema taarifa hiyo.

"Tunataka Wakili Peter Madeleka apelekwe mahakamani ndani ya muda mfupi kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi ili kuthibitisha kama kuna mashitaka dhidi yake,

Madai ya kukamatwa kwa wakili huyo yalizua taharuki baada ya kuvuja kwa taarifa za kundi la mtandao wa WhatsApp lililodaiwa kuwa la maofisa wa Uhamiaji kupanga mipango ya kumuua kwa kile kilichodaiwa anafichua siri za idara hiyo nyeti.

# Madereva bajaji, bodaboda waandamana kupinga zuio

**Na Waandishi Wetu**

KUNDI la madereva wa bajaji na bodaboda mkoani Dar es Salaam, jana waliandamana hadi ofisi ya Mkuu wa Mkoa wakipinga zuio lililowekwa la kufanya shughuli za usafiri katikati ya jiji.

Juzi, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilitoa tangazo la zuio la madereva bodaboda na bajaji kuingia katikati ya jiji wakiwa na abiria.

Hatua hiyo ilisababisha wao kuandamana hadi ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Saalm, hivyo kusababisha kufungwa kwa Barabara za Kawawa na Uhuru, wakipinga katazo hilo.

Hali hiyo ilimlazimu Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ngw'ilabuzu Ludigija, kuwatuliza kwa kuwaeleza kwamba Mkuu wa Mkoa, Amos Makala, angefika kuwasikiliza tatizo lao na hatimaye kukubali kuacha mgomo na kufunguliwa kwa barabara hiyo.

"Nikushukuru Mkuu wa Mkoa baada ya kukupigia na kukueleza hali ya hapa imekuwa mbaya, barabara yote ilifungwa hakukuwa na shughuli zozote zinazofanyika hasa ukizingatia Barabara ya Kawawa na Uhuru ni muhimu zinazotumiwa kwenda kwenye maeneo muhimu ya uzalishaji ikiwamo Kariakoo, ulisema unakuja," alisema Ludigija.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Mwenyekiti wa Umoja wa Wafanyabiashara wenye Ulemavu Mkoa wa Dar es Salaam, Juma Malecha, alisema kuna baadhi ya viongozi hawajui shida zao kama ni wenye ulemavu.

Malecha alisema makubaliano ya awali hayakuhusisha waziri wala mbunge bali yalikuwa miongoni mwao.

"Kiukweli tumeshtushwa na tumefadhaika sana eti yale tuliyokaa tukakubaliana kwamba sisi ambao ni wasakatonge katikati ya jiji, mtu ambaye si msaka tonge alione ni kero kwake. Tulichokitarajia waziri angemshauri mbunge alifanyie kazi apate majibu ya kumjibu," alisema.

**AGIZO LA WAZIRI**

Kabla ya barabara hizo kufungwa, Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alitoa maelekezo kwa Makalla kusimamia suala hilo la usitishwaji wa zuio hilo, ili kutoa nafasi ya kufanya tafakuri zaidi.

Bashungwa alimwelekeza Makalla kusimamia usitishwaji wa zuio hilo ili kutoa nafasi ya kufanya tafakuri zaidi.

Machi 31, mwaka huu, Nipashe ilifanya mahojiano na Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Jumanne Shauri, ambaye alisema mpango wao ni kuwatengea waendesha bajaji na bodaboda vituo maalum 15 ili kuwahudumia wateja wanaotoka katikati ya jiji kwenda nje.

Alisema vituo hivyo vitatengwa kwenye barabara zinazoingia katikati ya Jiji.

**BUNGE LAINGILIA**

Kutokana na sakata hilo, jana Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa (CCM) alilitaka Bunge kusimamisha shughuli zake na kujadili sakata hilo kama hoja ya dharura.

Baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'maswali' bungeni, mbunge huyo aliomba kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo hilo la dharura.

"Ni muhimu sana kwa sababu bodaboda wanabeba kundi kubwa la nguvu kazi ya vijana. Tumeona kwenye mitandao ya kijamii na wengine tumepigiwa simu kwamba kuna zuio bodaboda na bajaji kuingia katikati ya Jiji la Dar es Salaam.

"Mheshimiwa Spika, hata wewe juzi ulipokwenda Mbeya ulipokewa na kundi kubwa la vijana wa bodaboda na maeneo mengine tunawategemea. Jijini Dar es Salaam kumekuwa na sintofahamu kuhusu kundi hili, ninaomba wenzangu waniunge mkono tulijadili.

"Vijana hawa wamejiajiri na kusaidia familia zao kupitia biashara hii, hata sisi wabunge humu ndani tunawatumia, hili limetokea Dar es Salaam, siku zijazo litatokea Mbeya, Arusha, Dodoma na kwingine, ikikupendeza tulijadili hili suala humu," alitoa hoja Silaa.

Hata hivyo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akijibu hoja hiyo, alizuia kujadiliwa bungeni na badala yake akamtaka Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kushughulikia jambo hilo.

Spika Tulia alisema ili hoja ijadiliwe kwa dharura, ni lazima kiti chake kijiridhishe kuwa inafaa kuingia kwenye mjadala lakini kwa jambo hilo serikali ibebe dhamana ya kulishughulikia.

**MAKUBALIANO YAFIKIWA**

Katika jitihada za kutuliza maandamano hayo Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla amelazimika kufanya mawasiliano ya simu na Waziri Bashungwa na kumwelezea hali halisi ya maandamano hayo.

Baada ya mawasiliano hayo, Waziri Bashungwa ameridhia kuendelea kwa utaratibu uliokuwa ukitumika awali wa pikipiki na bajaji kuingia katikati ya mji kwa mujibu wa makubaliano na maridhiano ya pamoja yaliyokuwa yamewekwa baina ya waendesha bajaji wenye ulemavu na waendesha bodaboda.

Uamuzi huo ulipokewa kwa mikono miwili na waandamanaji hao ambao waliahidi kuendesha shughuli zao pasipo kuvunja makubaliano na utaratibu waliokuwa wamejiwekea awali kwa kuwa umehusisha na kukidhi matakwa ya pande zote.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (katikati), akisikiliza taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Benki ya Dunia, iliyowasilishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Dunia anayesimamia Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika, Dk. Taufila Nyamadzabo (hayupo pichani), kwenye Mkutano wa Magavana wa Benki hiyo, wakati wa Mikutano ya Kipupwe, jijini Washington DC, Marekani juzi. **PICHA: WFM**

# Ruwaichi, familia watoa neno maziko ya padri aliyefariki

**Na Jenifer Gilla**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Jude Thadaeus Ruwa'ichi, amesema uchunguzi juu ya chanzo cha kifo cha aliyekuwa Paroko wa Parokia ya Mbezi Mshikamano, Padri Francis Kangwa, unaendelea na atatoa taarifa utakapokamilika.

Wakati Askofu Mkuu akisema hayo, familia ya marehemu imesema haina dukuduku juu ya kifo cha ndugu yao na kwamba wanaamini ni mapenzi ya Mungu hivyo hawapendi kusikia tena habari hizo zikiendelea kuzungumzwa.

Ruwa'ichi aliyasema hayo jana katika Kituo cha Hija cha Pugu, wakati akiendesha misa ya mazishi ya padri huyo. Padri Francis alibainika amefariki dunia baada ya mwili wake kukutwa kwenye tangi la maji la katika nyumba ya mapadri iliyoko jengo la Ottoman, Dar es Salaam, Aprili 15, mwaka huu.

Askofu Mkuu Ruwa'ichi alisema hawajapata taarifa kuhusu mazingira ya kifo chake, hivyo wanasubiri uchunguzi wa polisi ukamilike.

"Na wale mnaododosa kwenye mtandao wa jamii mtakumbuka kwamba mwakilishi wa Jeshi la Polisi Dar es Salaam, alitoa taarifa ambayo ni tamko. Alitwambia kwamba uchunguzi bado unaendelea. Nami naomba niwaambie hata leo (jana) tunapokwenda kumzika Padri Francis hatujapata kauli ya mwisho kuhusu mazingira yote yaliyohusiana na kifo chake," alisema.

Kiongozi huyo alisema kumekuwa na maswali mengi juu ya chanzo cha kifo cha padri huyo na kukiri kuwa kwa sasa hana maelezo ya kutoa kuhusu suala hilo.

Alisema wamepata msiba mzito na wenye changamoto lakini hawana budi kuukubali kama wakristo na kuwaomba waumini kumwombea Padri Francis kwa Mungu ili apumzike kwa amani.

"Ndugu zangu nawaomba tukubali kwamba tunao msiba wenye changamoto, lakini pia tunao msiba ambao lazima tuukubali kama wakristo. Tuukabili kama wana wa Pasaka na kwa msingi huo nashukuru mliojitokeza kwa adhimisho hili la kumwombea na kumzika Padri Francis," alisema.

Ibada hiyo ya mazishi iliyotawaliwa na huzuni na vilio, ilihudhuriwa na mamia ya watu kutoka maeneo mbalimbali wakiwamo Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Polycarp Kardinari Pengo, zaidi ya mapadri 50 na waumini wa Kanisa Katoliki kutoka Parokia ya Mshikamano ambako Padri Francis alikuwa akihudumia. Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya familia, kaka wa marehemu, William Pangwa, alisema wanamshukuru Mungu kwa uhai wa Padri Francis na kuwa kifo ni mipango ya Mungu.

Alisema kaka yao aliyezaliwa mwaka 1971, alifanya kazi ya uinjilisti kwa miaka 20 mpaka umauti ulipomkuta na kwa miaka yote hiyo alikuwa mtu mwenye upendo kwa vijana na kila mara alitaka kuwasaidia.

"Alipenda kujitoa kwa watu na mara nyingi aliwatembelea wale wanaohitaji kuzungumza naye, mara ya mwisho kutembelea nyumbani tuliona baraka kubwa kupitia maisha yake na alihubiri kuhusu upendo wa Mungu na msamaha," alisema.

Naye Padri Richard Kagwa, kutoka Jimbo la Mpika Zambia ambaye pia ni kaka wa marehemu, alisema hawana malalamiko yoyote kuhusu kifo cha ndugu yao, hivyo wasingependa kusikia habari za kifo chake zikiendelea.

"Ujumbe kutoka katika familia yetu kama kaka yetu alivyosema, upo wazi kabisa kuwa tumekikubali kifo cha Padri Francis. Hatujali alikufa kwa njia gani, kwa nini alifariki (dunia), wapi na nani, hapana. Hatutaki kushindana na sauti ya Mungu," alisema.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA U J E N Z I , UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470DODOMA,
21.03.2022

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya **tarehe 19.04.2022 hadi 05.05.2022** kampuni ya Spedag Interfreight itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Holili kuelekea Moshi, gari hilo lenye namba za usajili: **KDB189J / ZG5310 KCW052Z / ZG3212**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - Mita 28.4 Upana - Mita 5.0 Kimo - Mita 5.6**

3. Njia itakayotumika: Holili hadi Moshi kupitia Soweto, gari litasafiri muda wa mchana tu ( **Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

216809602

## HABARI KITAIFA




Meneja Mkuu wa Mgodi wa North Mara, Apolinary Lyambiko (kushoto), akizungumza katika hafla ya kukabidhi msaada wa vipimo vya kisasa vya utambuzi wa magonjwa vilivyotolewa na kampuni ya Barrick kwa hospitali ya mkoa wa Mara, jana. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Mara, Ally Happi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CAG abaini mabilioni yako hatarini kupotea

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini mabilioni ya shilingi yako hatarini kupotea kutokana na kutokuwa na udhibiti mzuri wa usimamizi wa mikopo inayotolewa na halmashauri kwa makundi maalum.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwa 2020/21 iliyowasilishwa bungeni wiki iliyopita, CAG Charles Kichere anabainisha kuwa halmashauri 155 hazikukusanya Sh. bilioni 47.01 za marejesho ya mikopo iliyotolewa kwa makundi hayo.

Kwa mujibu wa CAG, hali iliyobainika katika ukaguzi wake wa mwaka 2020/21 ni mwendelezo wa kile alichokibaini katika miaka mitano iliyopita kuhusu mikopo hiyo.

| Mwaka | Hal. | Kisichorejeshwa | % |
|---|---|---|---|
| 2020/21 | 155 | 47,006,024,260 | 70 |
| 2019/20 | 130 | 27,790,189,049 | 65 |
| 2018/19 | 111 | 13,794,359,981 | 59 |
| 2017/18 | 90 | 10,044,453,656 | 59 |
| 2016/17 | 84 | 5,809,326,477 | 63 |

**Jedwali la mikopo isiyorejeshwa inayotolewa na serikali kwa makundi maalum kupitia asilimia 10 ya mapato ya halmashauri nchini. CHANZO: RIPOTI YA CAG, 2020/21.**

**UCHUNGUZI WA CAG**

Hata hivyo, CAG anabainisha kuwa katika kufuatilia uzingatiaji wa matakwa ya sheria iliyopo, alibaini kuwa, wanufaika wa vikundi katika mamlaka 155 za serikali za mitaa hawakurejesha Sh. bilioni 47.01 kama marejesho ya mkopo.

CAG pia anasema alibaini mamlaka 83 za serikali za mitaa hazikuchangia Sh. bilioni 6.68 katika mfuko kama inavyotakiwa kisheria, jambo ambalo linazuia azma ya serikali ya kuwawezesha kiuchumi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa lengo la kupunguza umaskini.

"Pia nilibaini mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 178.61 ilitolewa kwa vikundi visivyokuwa na sifa na Sh. bilioni 1.24 hazikuhamishwa kutoka akaunti za amana za mamlaka 11 za serikali za mitaa kwenda akaunti maalum ya mfuko, kinyume cha Kanuni ya 22 (1) na (2) ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu," anasema.

Anazitaja halmashauri ambazo hazikuhamishia Sh. bilioni 1.24 katika akaunti maalumu za mikopo ni: Ushetu (Sh. 308,528,550); Bahi (Sh. 54,222,488); Iringa (Sh. 236,486,588); Busega (Sh. 49,090,000); Nanyumbu (Sh. 179,268,173); Momba (Sh. 41,795,000); Kilolo (Sh. 122,596,622); Gairo (Sh. 38,679,672); Rungwe (Sh. 115,777,111); Ileje (Sh. 32,043,700); na Sengerema (Sh. 59,511,900).

**SHIDA ILIKOJIFICHA**

CAG anabainisha kuwa kutorejeshwa kwa mikopo hiyo kunatokana na kutokuwa na udhibiti mzuri wa usimamizi wa mikopo, akifafanua kuwa mamlaka za serikali za mitaa husika zilitoa mikopo kabla ya kufanya uchambuzi wa kina wa historia ya ulipaji wa kikundi na kupitia mapendekezo ya mradi husika ili kuhakikisha kuwa kikundi kina uwezo wa kurejesha mkopo kwa wakati.

Vilevile, CAG anasema amebaini hakuna ufuatiliaji wa karibu wa kukusanya marejesho ya mikopo ambayo bado haijalipwa kutoka kwenye vikundi. Anasema ni dhahiri kuwa kutorejeshwa mikopo kunaweza kuathiri mfuko, hivyo kuufanya usiwe endelevu.

Ili kufikia lengo na uendelevu wa mfuko, CAG anasisitiza mamlaka za serikali za mitaa kufanya tathmini kabla ya kutoa mikopo na kuweka juhudi zaidi katika kukusanya madeni ambayo bado hayajalipwa.

Anaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ianzishe hatua madhubuti za kurejesha mikopo kwa kuhusisha wataalamu wa usimamizi wa mikopo ambao watahimiza uzingatiaji wa urejeshaji wa mikopo kwa hiari ili kufikia ukuaji endelevu wa mfuko.

CAG pia anabainisha kuwa tathmini aliyoifanya katika akaunti za benki za biashara ambako mamlaka za serikali za mitaa hutunza fedha za mfuko, ilibainisha Sh. milioni 156.23 za mfuko zilizimbikizwa katika akaunti kwa zaidi ya mwaka mmoja bila kukopeshwa kwa wanufaika pasipokuwa na sababu za msingi.

Halmashauri zilizokuwa na bakaa ya muda mrefu katika benki za biashara ni za wilaya za Mpwapwa (Sh. 108,703,450) na Nyasa (Sh. 47,530,700).

CAG anataja dosari nyingine katika mikopo hiyo ni kutoshirikishwa kwa wataalamu wa usimamizi wa mikopo katika mchakato wa utoaji na urejeshwaji wa mikopo.

## Wabunge waibana serikali kutoa ajira

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imesema katika mwaka wa fedha 2022/23 itaajiri watumishi wapya 30,000 katika kada mbalimbali zikiwamo za afya na elimu watakaoigharimu zaidi ya Sh. bilioni 120.

Vilevile, serikali inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi 120,210 wataolipwa Sh. bilioni 42 na watumishi 8,080 waliotengewa nafasi za kubadilishwa vyeo na kuigharimu serikali Sh. bilioni 2.21 kulingana na maelekezo yatakayotolewa.

Hata hivyo, baadhi ya wabunge wameitaka serikali kuja na mkakati wa kutatua tatizo la uhaba wa watumishi kwenye sekta mbalimbali nchini ili kutoa huduma bora kwa wananchi, wakifafanua kuwa ajira mpya 30,000 zinazotarajiwa kutolewa mwakani, zinakwenda kupunguza tatizo kwa kiwango kidogo.

Mpango wa kutoa ajira hizo ulibainishwa jana bungeni jijini hapa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Aliliomba Bunge kuidhinishiwa zaidi ya Sh. bilioni 850 kwa ajili ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka ujao wa fedha. Kati yake, Sh. bilioni 670 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 181 ni za matumizi ya miradi ya maendeleo.

Jenista alisema, pia watachambua na kuhakiki madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma kwa kadiri yatakavyowasilishwa, Sh. bilioni 103.9 zimetengwa kwa ajili ya malipo ya madai yatakayoidhinishwa.

"Pia, jumla ya miradi 6,900 ya jamii na ya kutoa ajira za muda itatekelezwa katika ngazi ya vijiji/mitaa/shahia 6,500 na inategemewa kutoa ajira za muda kwa walengwa 550,000," alisema.

**WABUNGE WALALAMA**

Wakichangia hoja hiyo, baadhi ya wabunge waliitaka serikali kuwa na mkakati wa kutatua kero ya uhaba wa watumishi nchini. Prof. Kitila Mkumbo, Mbunge wa Ubungo (CCM), alisema watumishi wa umma ni injini ya utekelezaji wa sera, sheria na mipango ya serikali, hivyo kuna haja kuwa nao wa kutosha.

Alisema kwa sasa kuna tatizo kubwa la uhaba wa watumishi kwenye maeneo mbalimbali nchini, akifafanua kuwa kwenye shule za msingi na sekondari mahitaji ya walimu ni 433,992, lakini waliopo ni 258,291, hivyo kuwa na upungufu wa walimu 175,701 (asilimia 40).

Kwa upande wa Sekta ya Afya, Prof. Mkumbo alisema kuna watumishi 98,987 ilhali mahitaji ni kuwa nao 208,232, hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 109,295, sawa na asilimia 52.5.

Alisema kuwa Sekta ya Kilimo ambayo ni muhimu katika uzalishaji, inahitaji maofisa ugani 20,000, lakini waliopo ni 6,600. Kwa ujumla, Prof. Mkumbo alisema upungufu wa watumishi kwa sasa nchini ni zaidi ya milioni 1.2.

Mbunge wa Viti Maalum, Ester Bulaya, pia alisema uhaba wa watumishi wa umma nchini ni mkubwa, akitolea mfano Bunda yenye uhaba wa watumishi zaidi ya 900.

Mbunge wa Viti Maalum, Leah Komanya (CCM), aliitaka serikali kuhakikisha nafasi za ajira mpya 32,000 zilizotangazwa zinaelekezwa kwenye wilaya zenye uhaba mkubwa, akiitolea mfano Wilaya ya Meatu ambayo ndani ya miaka mitano watumishi 232 wamehama na wengine 156 wamestaafu.

Mbunge wa Mlalo, Rashid Shangazi (CCM), alisema kuna faida kubwa kupandisha watendaji madaraja kwa mkupuo, wenye sifa wabainishwe na kupewa stahiki zao.

TANGAZO

NMB Karibu yako

Tangazo hili limeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)

**NMB BANK PLC ("NMB")**
**(Imesajiliwa nchini Tanzania chini ya Sheria ya kampuni ya Tanzania ya mwaka 2002 kama kampuni yenye dhima ya ukomo, (cheti cha usajili namba 32699))**

# TANGAZO KWA UMMA
# MATOKEO YA MAUZO YA HATIFUNGANI YA JASIRI YA BENKI YA NMB (NMB JASIRI BOND)

Benki ya NMB ("NMB") inatoa taarifa kwa umma kuwa mnamo tarehe 03 Februari 2022 Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ilitoa idhini kwa NMB kuuza hatifungani ya Jasiri yenye thamani ya shilingi za kitanzania bilioni 25 ikiwa ni toleo la nne ya programu ya hatifungani ya NMB yenye jumla ya shilingi za kitanzania billioni 200. Hatifungani hii ni ya kwanza Afrika Mashariki ambayo ina mguso na matokeo chanya kwa Jamii yaani Social Impact Bond na imekidhi matakwa ya Kanuni za Jumuiya ya Kimataifa ya Masoko ya Mitaji (International Capital Markets Association - ICMA) na kuidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana.

## MATOKEO YA MAUZO YA HATIFUNGANI YA JASIRI

Mauzo ya hatifungani ya Jasiri ya Benki ya NMB yalifunguliwa tarehe 07 Februari 2022 na kufungwa tarehe 21 Machi 2022, ambapo Benki ya NMB ilifanikiwa kupata kiasi cha shilingi za kitanzania bilioni 74.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 25 zilizotarajiwa kukusanywa, sawa na mafanikio ya asilimia 297.

## IDHINI YA KUONGEZA KIASI

NMB ilipata idhini kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kukusanya kiasi cha shilingi za kitanzania bilioni 25 na ongezeko la hadi shilingi bilioni 15. Kufuatia kiasi kilichopatikana kufikia shilingi za kitanzania bilioni 74.3 ikiwa ni mafanikio ya asilimia 297, NMB imeomba na kupata idhini tarehe 11 Aprili 2022 kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), kupokea maombi yote ya mauzo ya hatifungani ya Jasiri.

## MUHTASARI WA HATIFUNGANI YA NMB JASIRI

Muhtasari wa takwimu muhimu za mauzo ni kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **Mtoaji** | NMB Bank Plc |
| **Maelezo** | Programu ya hatifungani za muda wa kati za NMB |
| **Muda** | Miaka 3 |
| **Aina ya Hatifungani** | Daraja la kwanza, isiyokuwa na dhamana, kiwango cha riba kisichobadilika |
| **Toleo la** | 04 |
| **Namba ya Kumbukumbu** | NMB-FXD04/2022/03* |
| * Ufafanuzi wa namba ya kumbukumbu: NMB – NMB Bank PLC; FXD04 – Hatifungani ya toleo la nne lenye kiwango cha riba kisichobadilika; 2022 – mwaka wa kutolewa; 3 – muda wa hatifungani | |
| **Tarehe ya Kutoa** | 28 Machi 2022 |
| **Jumla ya kiwango kilichotolewa chenye marekebisho (TSH.)** | 25,000,000,000 (na ongezeko la hadi shilingi 49,268,740,000) |
| **Jumla ya mtaji uliokusanywa (TSH.)** | 74,268,740,000 |
| **Kiwango cha matokeo (%)** | 297% |
| **Jumla ya kiasi kilichokubaliwa (TSH.)** | 74,268,740,000 |
| **Kiwango cha riba** | 8.5% kwa mwaka |
| **Bei ya Hatifungani** | Ni ile iliyotangazwa |
| **Kiwango cha chini** | Shilingi 500,000 (pamoja na nyongeza ya mafungu ya shilingi 10,000) |
| **Matumizi ya Mtaji uliopatikana** | Mtaji uliopatikana kupitia mauzo ya hatifungani ya Jasiri utatumika kutoa mikopo kwa biashara ndogo na za kati zinazomilikiwa na wanawake au zile ambazo bidhaa au huduma zake zinamgusa mwanamke moja kwa moja. |

## SERA YA UGAWAJI

Kutokana na maombi zaidi kupokelewa, Benki imeomba na kupata idhini ya CMSA:

i. kutekeleza kiwango cha nyongeza kwa kuongeza kiwango cha ugawaji wa hatifungani kutoka shilingi 40,000,000,000 hadi shilingi 74,268,740,000; na
ii. kukubali maombi yote sahihi yaliyopokelewa. Waombaji wote watapokea asilimia mia (100%) ya maombi yao.

## MAELEZO YA ZIADA

Endapo mwombaji wa Hatifungani atahitaji ufafanuzi, anashauriwa kuwasiliana na dalali wa soko la hisa au NMB kupitia nmbbond@nmbbank.co.tz au +255 22 2322000

## TAREHE ZA MATUKIO MUHIMU

Tafadhali angalia tarehe zilizopendekezwa kufuatia ufungaji wa ofa:

| Maelezo | Tarehe |
|---|---|
| Tarehe ya kutaarifiwa (kupitia baruapepe/ simu) | Saa 10.00 jioni, Alhamisi ya tarehe 14 Aprili 2022 |
| Tarehe ya Malipo (kwa taasisi za uwekezaji zenye sifa tu) | saa 8.00 mchana, Jumatatu ya tarehe 28 Machi 2022 |
| Tarehe ya Kutoa | Jumatatu ya tarehe 28 Machi 2022 |
| Tarehe ya kuweka katika akaunti ya CDS | kabla au mpaka Jumatano ya tarehe 27 Aprili 2022 |
| Tarehe ya kuorodhesha hatifungani kwenye soko la hisa | Alhamisi ya tarehe 28 Aprili 2022 |

## SHUKRANI

Menejimenti ya benki ya NMB inatoa shukrani za dhati kwa taasisi zote zilizofanikisha uuzwaji wa hatifungani ya NMB Jasiri. Taasisi hizi ni pamoja na Bodi na Uongozi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); Bodi na Uongozi wa Soko la Hisa la Dar Es Salaam; Dalali Mfadhili wa benki ya NMB, Orbit Securities Company Limited; FSD Africa iliyotoa ushauri wa kitaalamu kwa benki ya NMB kwenye Muongozo wa Hati Fungani zenye mguso kwa Jamii kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni (Social Bond Principles) ya Jumuiya ya Kimataifa ya Masoko ya Mitaji (ICMA); na Sustainalytics iliyotoa maoni ya mtu wa pili kuhusu Muongozo huo.

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu,**
**NMB Bank PLC,**
**Barabara ya Ohio/Ali Hassan Mwinyi,**
**S.L.P 9213, Dar es salaam, Tanzania**

**Tarehe: 22 Aprili 2022**

216816802

www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ujenzi, ukarabati wa barabara sasa upewe kipaumbele endelevu

**BARABARA** ni miundombinu muhimu sana katika uchumi na maendeleo ya jamii, hivyo kila wakati kuwa kipaumbele kikubwa kwa wananchi.

Umuhimu wa barabara unadhihirishwa na malalamiko yanayotolewa na wananchi katika maeneo takribani yote nchini kwenye mikutano ya hadhara wanapokuwa wakizungumza na viongozi mbalimbali wakiwamo mawaziri na wawakilishi wao (madiwani, wabunge na wawakilishi).

Wamekuwa wakilalamikia kukosa au kupata huduma hizo zikiwamo za elimu na afya kwa taabu kutokana na ubovu wa barabara, hivyo kuiomba serikali kuhakikisha inazijenga au kuzikarabati mara kwa mara. Hakika barabara ni kikwazo kwa wengi, licha ya jitihada za serikali katika kukabiliana nalo.

Kadhalika, kwenye mikutano ya mabaraza ya madiwani, wabunge na baraza la wawakilishi moja ya huduma ambazo zimekuwa zikiibua mijadala mingi ni barabara, huku madiwani, wabunge na wawakilishi wakipaza sauti kuihoji serikali ni kwa nini haijengi barabara katika maeneo yao na ni lini itafanya hivyo?

Ni maswali ambayo yamekuwa yakiwafanya wahusika kama wakurugenzi na mawaziri kutoa majibu ambayo mara nyingi ni ahadi za kutegemea uwezo wa serikali kifedha pamoja na mipango ya muda mrefu.

Kutokana na kujirudiarudia kwa suala la barabara katika Mkutano wa Bunge unaoendelea, Spika Dk. Tulia Ackson mapema wiki hii alitoa ushauri kwa serikali, pengine baada ya kuona ukubwa wa tatizo hilo.

Jumanne, Dk. Tulia aliishauri serikali kuweka utaratibu wa kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo madogo ya barabara kuepuka gharama kubwa za kuzitengeneza upya.

Ushauri wake ulitokana na swali la nyongeza alilouliza mbunge mmoja wa viti maalum, ambaye alisema serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi katika kujenga barabara, lakini baada ya muda mfupi zinaharibika au kuota nyasi.

Mbunge huyo alihoji kwamba serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za matengenezo ya barabara hizo ili kuzinusuru.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alisema barabara nyingi za changarawe na vumbi hazidumu kwa muda mrefu na hutengewa fedha kwa ajili ya matengenezo kila mwaka, na kwamba azma ya serikali ni kujenga barabara zote kwa kiwango cha lami. Kasekenya pia alisema ujenzi wa barabara hizo ni gharama na zinategemea upatikanaji wa fedha.

Kutokana na majibu hayo, Spika Tulia aliingilia kati na kusema fedha nyingi zimekuwa zikitumika kujenga barabara hizo, lakini matengenezo huwa hayafanyiki, na kusababisha kuharibika kwa kiwango kikubwa, hivyo kulazimisha kuondoa lami na kujengwa upya.

Tunakubaliana na ushauri wa Spika Tulia kwa serikali kuhusu utaratibu wa kutenga fedha za matengenezo madogo ya barabara kuepukana na baadae kutumika fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo, na wakati mwingine kuchelewa kupata fedha hizo kuwa shida.


Tunaishauri serikali kuanzisha utaratibu huo kwa kuhakikisha Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) zinapatiwa fedha kwa wakati kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao.

Suala lingine linalopaswa kupewa kipaumbele ni kuhakikisha kwamba barabara nyingi zilizoko chini ya TARURA zinafanyiwa ukarabati kwa wakati mwafaka hususan baada ya kipindi cha mvua zinapokuwa zimeharibika.

Tunasema hivyo kutokana na utaratibu mbovu wa barabara hizo kufanyiwa ukarabati wakati wa mvua za masika au vuli, hivyo kupoteza maana halisi ya ukarabati.

Kufanya ukarabati kabla kidogo au wakati wa mvua kunatoa tafsiri kuwa wahusika wana maslahi binafsi badala ya maslahi ya wananchi ambao wanahitaji barabara hizo zipitike kwa kipindi kirefu bila shida.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wamachinga wasipoteze fursa hii waliyopewa na serikali yetu

Na Sabato Kasika

**SERIKALI** na wamachinga wamekutana katika kikao cha pamoja kwa lengo la kuweka mikakati mbalimbali ya kuboresha shughuli zao, ili hatimaye watoke kwenye umachinga wawe na biashara kubwa.

Kikao hicho kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma, kinaweza kuwa msingi wa kuimarisha biashara yao iwapo wafanyabiashara hao watazingatia na kutekeleza kwa vitendo maazimio waliyofikia.

Baadhi ya maazimio hayo ni Wizara hiyo na SHIUMA kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI kuhakikisha mamlaka za serikali za mitaa kupanga na kuweka miundombinu wezeshi katika maeneo ya shughuli za wamachinga.

Hatua hiyo inapaswa kufanyika kwa kushirikisha viongozi wa wamachinga wa eneo husika, kuandaa kanzidata ya wamachinga na wizara kutembelea maeneo ya masoko ya wafanyabiashara hao ili kutatua changamoto zilizopo.

> **Hatua hiyo inapaswa kufanyika kwa kushirikisha viongozi wa wamachinga wa eneo husika, kuandaa kanzidata ya wamachinga na wizara kutembelea maeneo ya masoko ya wafanyabiashara hao ili kutatua changamoto zilizopo.**

Mbali na hilo, wizara pia inatakiwa kuboresha madawati ya kushughulikia masuala ya wamachinga kwa kushirikiana na TAMISEMI hadi halmashauri, ili kutatua changamoto katika maeneo yao.

Aidha, azimio lingine ni sheria ndogo zinazowahusu wamachinga zinatakiwa kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ili wazielewe kirahisi na watimize wajibu wao bila msuguano na serikali.

Kutokana na maazimio hayo, ninaamini kwamba, yatasaidia kupunguza kero ambazo zimekuwa zikisababishwa na wamachinga mitaani, na hivyo kufanya shughuli kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula aliyeongoza kikao hicho, anawataka wamachinga kushirikiana na serikali kutekeleza maazimio hayo, kwa maslahi yao na taifa kwa ujumla.

Ninaamini kwamba kuyatekeleza, kutaondoa sintofahamu kwenye suala la uhamishaji wa wamachinga kutoka maeneo yasiyo rasmi kwenda katika masoko waliyotengewa na serikali, ambao baadhi yao hawajahama.

Miongoni mwa maeneo hayo ni Mbezi Luis Dar es Salaam, ambako wamachinga wanaendelea na biashara kando ya barabara, juu ya mitaro ya maji ya mvua hali ambayo ni hatari kwa usalama wao.

Sababu kubwa ya kuendelea na biashara katika maeneo waliyoondolewa, wanadai ni ukosefu wa maeneo katika masoko, hali inayowalazimu kuuza bidhaa zao hata katika mazingira hatarishi.

Wakati wakisema hayo, wengine hudai kuwa katika masoko mapya hakuna wateja, hivyo wanaona ni bora waendelee kufanya biashara kule walikoondolewa kwa madai kwamba kuna wateja wengi.

Maelezo hayo yanaweza kutumiwa na mamlaka husika kupata ukweli na kuweka mikakati ya kuhakikisha wamachinga wanafanya biashara zao katika maeneo rasmi waliyotengewa na kuepuka mtindo wa kwenda huku na kule.

Nionavyo, serikali ina nia ya kuhakikisha kundi hilo linapata maendeleo kupitia shughuli zake, hivyo kikao cha Dodoma cha kuwajengea uelewa wa mambo muhimu ikiwamo sheria, kanuni na taratibu za serikali ni cha muhimu.

Cha msingi ni kuboresha miundombinu katika masoko yao ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi, kwani wana mchango kwenye ajira na inawezekana ndiyo maana Rais Samia Suluhu Hassan akawaweka katika kundi maalum.

## HABARI KITAIFA

# Ridhiwani akemea watumishi wala rushwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA



NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete (pichani),amewataka watumishi wa wizara hiyo kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia haki na kujiepusha na kuomba na kupokea rushwa.

Kikwete alibainisha hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara hiyo uliofanyika kwa siku moja jijini Dodoma.

Alisema watumishi wanatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia haki wakati wa kuhudumia wananchi na kuacha kujihusisha na vitendo vya rushwa ambavyo vimekuwa vikichangia kwa kiasi kikubwa malalamiko kutoka kwa wananchi.

"Mnapaswa kuhakikisha kuwa katika utekelezaji wa majukumu yenu ya kila siku mnatenda haki kwa wananchi bila kumwonea mtu na wala msijihusishe na masuala ya kuomba na kupokea rushwa ambayo yanaitia aibu serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Nisisitize kuondoa uonevu katika utendaji kazi hasa mfumo kandamizi katika usimamizi wa mipango ya ardhi mfano upimaji unapofanyika kwa makubaliano ya kuchukua asilimia fulani ya viwanja vya wananchi lakini wakati huo huo kuwachaji tena wananchi kwa kulipa gharama za upimaji," alisisitiza Kikwete.

Alisema utaratibu huo haukubaliki na hautowi taswira nzuri kwa wizara hiyo na kuwakumbusha kuwa tayari Rais ameutangazia umma kuwa Agosti 23, mwaka huu, itakuwa siku ya Sensa ya Watu na Makazi.

"Nawaomba kujiandaa kikamilifu na kwa kuzingatia wizara yetu ni mdau wa suala hilo, tujipange kikalimifu ili kutimiza lengo lililokusudiwa sisi viongozi wenu wakuu wa wizara tuko tayari na hatutamfumbia macho yeyote atakayekwamisha ushiriki wa wizara kwenye sensa," alisema

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Allan Kijazi, alisema pamoja na mambo mengine, baraza hilo ni mahususi kwa ajili ya kujadili makisio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka 2022/23 ikiwa ni hatua muhimu kuelekea kuwasilishwa bungeni hivi karibuni.

# CCM yajitosa foleni barabarani Kigamboni

**Na Romana Mallya**



CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema kinakwenda kujadiliana na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili kutafuta suluhu ya foleni za magari hususani malori wilaya ya Kigamboni inayosababishwa na miundombinu mibovu.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo (pichani) wakati akiwa katika ziara yake akifuatilia mchakato wa uchaguzi ngazi ya mashina wilayani humo.

"Tunaona kasi ya ukuaji wa wilaya ya Kigamboni na magari yamekuwa mengi na yanachukua hadi muda wa masaa matatu kufika na kutoka Kurasini, naondoka na tatizo hili ninakwenda kuongea na TANROADS na TARURA kuona namna ya kuboresha barabara hizi kwa sababu Kigamboni ni lango la uchumi," alisema.

Alisema wanakwenda kuweka msukumo kuhakikisha miundombinu ya barabara na vivuko wilayani humo vinaboreshwa kwa sababu asilimia 90 ya bidhaa ya mafuta hutoka huko.

Pia alisema bado wanajipanga ili kuja na suluhu ya kudumu ya kuboresha vivuko.

Kiongozi huyo ameziagiza mamlaka husika kutengeneza vivuko vilivyoharibika kwani vivuko hivyo siyo anasa bali ni huduma.

Kadhalika alisema matatizo yaliyopo katika daraja la Julius Nyerere walishayapokea na wanaendelea kuyafanyia kazi.

Chongolo alisema, "Matatizo yote tunayabeba na tunaiangalia Kigamboni kwa jicho la tatu, tutajenga barabara kuanzia kibada itakatisha Kisarawe II ,Pemba Mnazi hadi Mbagala."

Mwenyekiti wa Chama hicho Mkoa wa Dar es Salaam, Kate Kamba alisema, "Tutumie fursa ya uwapo wa maeneo Kigamboni kujiwekeza kwa kujenga hoteli kubwa kuongeza vitega uchumi kwa sababu vingi tunavyomiliki kwa sasa vilijengwa chini ya utawala wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere."


VisionFund TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

## VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

## VACANCIES

VisionFund Tanzania Microfinance Bank Ltd (VFT MFB) formerly known as SEDA is a fast growing and reputable **Micro Finance Bank (MFB),** that has a loan book of approximately TZS. 20 billion and more than 30,000 client base, more than5,000 of whom are small holder farmers.

VFT-MFB is seeking to employ a dynamic and committed Tanzanian young man or woman who has a passion for people's economic development to fill in the vacant positions detailed here below;

**Work Reference No. 005/22**
**Position: Recovery Manager**
**Reporting to: Chief Operations Officer (COO)**

**Responsibility:**
- To ensure an efficient performance of the Recovery Unit and direct supervision of the recovery officers and other stakeholders in the recovery activities chain.

**Main tasks (Not Exhaustive):**
- Ensures efficient performance of the Recovery Unit
- Coordination of the Recovery Unit work with other units/departments or agents
- Coordinates Recovery Unit personnel plan
- Direct supervision of the recovery officers
- To exchange information with the Recovery Officers, Regional Managers, Business Center Managers and other stakeholders in the recovery activities chain.
- To take part on the recruitment of Recovery Interns and Debt Collectors
- To develop Recovery Plans in consultation with Chief Operations Officer
- To prepare reports to be submitted to the Chief Operations Officers and other Heads of department as the need may arise.

**Education/Experience**
- Bachelor Degree in; Business Administration, Accounting, Finance and Economics
- A good background in legal knowledge and practice in recovery matters is an added advantage
- Very good analytical & reporting skills
- 5 years' experience in credit management and loan recovery experience
- Experience of at least 5 years in working direct with Saving Groups, 2 of which must be at the Managerial/Supervisory position.

**Work reference no. 006/22**
**Position: Recovery Officer**
**Reporting to: Recovery Manager**

**Responsibility:**

- Responsible for Assisting/ supporting the Recovery Manager in facilitating all recovery related issues in accordance with VFT - MFB's policies.

**Main tasks**

1. Ensure proper documentation for loan recovery
2. Ensure collection of outstanding non-performance loan past 90 days
3. Ensure collection of outstanding written off loans.
4. Monitoring and coordination of all debt collector's activities
5. Ensure compliance of Loan Officers & BCM on proper procedures in recovery
6. Reporting

**Education/Experience**

- Bachelor Degree in; Business Administration, Accounting, Finance and Economics
- 3 years' work experience in recovery activities in the Banking and Financial Institutions
- Very good knowledge on analyzing financial information
- Very good analytical & report writing skills
- Proficient in Microsoft office application
- Model and demonstrate effective Christianity maturity.

**About our working environment & remuneration.**

VisionFund Tanzania Microfinance Bank has a calm and harmonious working environment where staffs are highly valued. Good work is recognized and rewarded accordingly and there is an opportunity to grow professionally and spiritually.

**Mode of Application:**
Interested and suitably qualified individuals should;

1. Forward their application letter, attaching certified copies of their academic and professional certificates; detailed CV's with three referees to **vftHRstaff@vftz.co.tz.**
   OR:
2. Physically send their applications through the postal address below:

   **VisionFund Tanzania Microfinance Bank Limited,**
   **AICC Building, Serengeti Wing, 5th Floor**
   **P.O. Box 1546,**
   **Arusha, TANZANIA.**

3. All applications should be addressed to;

   **The Chief Executive Officer,**
   **VisionFund Tanzania Microfinance Bank Limited**
   **P.O. Box 1546,**
   **Arusha, TANZANIA.**

4. The position should be the subject of the email application.
5. The deadline for the application is on **4th May, 2022.**

**N.B. Only short-listed candidates will be contacted.**

**Disclaimer**
VisionFund Tanzania Microfinance Bank would like to inform the general public that it has not engaged any consultant/agent to conduct recruitment on its behalf.




Ofisa Tarafa ya Nyanchenche, wilayani Sengerema, mkoani Mwanza, Happiness Juma (kulia), akipokea karatasi ya maelezo ya msaada wa choo cha matundu sita kutoka kwa Meneja Uhusiano wa kampuni ya uchimbaji madini ya OreCorp, John Bwana, wakati wa hafla ya kukabidhi choo hicho kilichojengwa kwenye Shule ya Msingi Chikomelo katika kijiji cha Nyasibo wilayani humo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakiwa kukataa kunyanyaswa kijinsia

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Msaada wa Kisheria (KPC), Catherine Mlenga, amesema ili wanawake wafanye shughuli zao kwa ufanisi, wanatakiwa kutokukubali kunyanyasika kwenye familia.

Badala yake amewataka wajenge ujasiri wakutoa taarifa pindi wanapofanyiwa vitendo vya ukatili.

Amesema baadhi ya wanawake wanafanya biashara wakiwa na msongo wa mawazo hali inayosababisha biashara kukwama na kwamba endapo wataendelea kuwa kimya, watazidi kudidimia kiuchumi na kukosa maendeleo.

Mkurugenzi huyo alibainisha hayo jana mjini Kibaha wakati wa uzinduzi wa mfuko wa uwezeshaji wa kukopeshana kwa riba nafuu katika kata ya Picha ya Ndege.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Picha ya Ndege, Zawadi Salim, alisema kikwazo wanachokabiliana nacho wanawake ni baadhi yao kutoona umuhimu wa kujiunga kwenye majukwaa hayo.

Salim alisema moja ya malengo yao ni kuwa na biashara za pamoja ambazo zitatengenezwa kwa kuzingatia ubora na kuzipeleka sokoni ili zishindane na nyingine.

Katibu wa Jukwaa hilo, Akothlilian Bake, alisema wamezindua mfuko wa uwezeshaji wa kukopeshana kwa riba nafuu wenye lengo la kuwainua wanawake kiuchumi.

Alisema malengo mengine ni kuwaunganisha wanachama na taasisi za mikopo na kuwatafutia masoko ya biashara zao.

Diwani wa Viti Maalum Halmashauri ya Mji Kibaha, Shufaa Bashari, aliwataka wajasiriamali hao kujiamini kuwa wanaweza kwa kujiongezea kipato badala ya kusubiri kuletewa nyumbani.

# Shule yapigwa jeki ujenzi wa vyoo sita

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Msingi Chikomelo iliyopo Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza yenye wanafunzi 120, imekabidhiwa vyoo sita na kampuni ya OreCorp Tanzania ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali katika sekta ya elimu.

Akizungumza juzi na Nipashe baada ya kukabidhi msaada huo, Meneja Mkuu wa kampuni hiyo, Damien Valente, alisema ujenzi wa vyoo hivyo ulianza Machi 17, mwaka huu na umemalizika Jumamosi iliyopita.

Valente alisema OreCorp Tanzania imekuwa ikiiunga mkono jamii kwenye suala la miundombinu muhimu.

"Tunashukuru mamlaka za Wilaya ya Sengerema kwa kuendelea kutupa mwongozo na ushirikiano wao katika miradi yetu ya kuimarisha jamii," alishukuru.

Ofisa Tarafa wa Nyancheche wilayani Sengerema, Happiness Juma alisema kuwa msaada huo ni sehemu ya matunda ya serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amedhihirisha kuwatambua wawekezaji wanaokuja Tanzania kuwekeza.

Mbali ya kutoa msaada wa vyoo shuleni hapo, mwezi Julai mwaka jana kampuni hiyo ilianza ujenzi wa madarasa matatu, vyoo na madawati katika Shule ya Sekondari ya Ngoma na kukabidhi mwezi Februari, mwaka huu.

Kampuni hiyo inajishughulisha na ujenzi wa mradi wa dhahabu wa Nyanzaga uliopo wilayani humo ambao unakadiriwa kuwa na wakia milioni tatu za dhahabu na utazalisha kiasi cha wakia 200,000 (tani sita) za dhahabu kwa mwaka na ujenzi

# RUWASA yajitoa kuokoa wananchi kuliwa na mamba

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Kibaha imeeleza mipango yake ya kufikisha maji katika kitongoji cha Kigogo ili kunusuru maisha ya wananchi ambao wako hatarini kuliwa na mamba kutokana na kutumia maji kutoka Mto Ruvu.

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Kibaha, Mhandisi Debora Kanyika, alisema jana kuwa kwa sasa kuna mradi mkubwa unaotekelezwa katika kijiji cha Kimara Misale chenye vitongoji viwili, kikiwamo cha Kigogo.

Kanyika alisema mradi wa maji katika kijiji hicho, ulianza kutekelezwa Januari, mwaka huu, na unatarajiwa kukamilika Julai, mwaka huu huku akibainisha kuwa gharama za mradi huo ni Sh. 498,709,539.89 za UVIKO-19.

"Kupitia mradi wa maji wa kijiji cha Kimara Misale, RUWASA itafikisha huduma katika kitongoji cha Kigogo, hivyo kuondoa adha iliyopo ya wananchi kukosa maji na kulazimika kutumia maji ya Mto Ruvu jambo ambalo ni hatari kwao kutokana na tishio la mamba," alisema Kanyika.

Kwa sasa, alisema ujenzi wa mnara wa tangi lenye ujazo wa lita 50,000 wenye kimo cha mita 12 umefikia mita nane na kazi hiyo inaendelea.

Kanyika pia alisema vituo vinane vya kuchotea maji vimejengwa na viko kwenye hatua ya umaliziaji , huku ujenzi wa nyumba ya mitambo ukiendelea.

Alisema kwa sasa kikwazo wanachokabiliana nacho katika utekelezaji wa mradi huo ni mvua ambazo zinasababisha wakati mwingine wataalamu kukwama kufika eneo la ujenzi kutokana na hali ya barabara.

Mpango wa mradi wa maji wa kufika katika kitongoji cha Kigogo utakapomalizika, utaondoa kikwazo kilichopo sasa cha wananchi kutegemea maji katika Mto Ruvu. Hivi karibuni ilielezwa kuwa watu sita wameliwa na mamba kwa nyakati tofauti walipokwenda kuchota maji katika mto huo.

HABARI KITAIFA

# NIC yajipanga kutoa gawio la bil.1.5/-

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Bima la Taifa (NIC), limesema linatarajia kuanza kutoa gawio kwa serikali Sh. bilioni 1.5 mwezi huu.

Hayo yalielezwa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa NIC, Dk. Elirehema Doriye, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema licha ya NIC kutokutoa gawio kwa miaka mingi, mara ya mwisho ilitoa gawio la Sh. bilioni 1.7 mwaka 2017, mwezi huu linatarajia kutoa kwa mara ya pili.

Dk.Doriye alisema kutokana na faida kubwa ambayo shirika hilo limepata, kwa sasa Sh. Bilioni 12.5 zimetengwa kwa ajili ya kuongeza mtaji wa kuimarisha shirika. Alisema kwa sasa NIC limejipanga vizuri kuimarisha utendaji na kutoa huduma bora kwa wateja.

"Katika kuimarisha shirika na kuhakikisha kuwa linaweza kufanya biashara kubwa na kuliongezea uwezo mkubwa ili liwe bora zaidi kimtaji na kiutendaji ndiyo maana kikao cha bodi kimeamua Sh.bilioni 12.5 zitumike kama mtaji," alisema Dk. Doriye.

Aliongeza kuwa fedha hizo ni sehemu ya faida ya shirika ya Sh. bilioni 13.55, huku akieleza kuwa NIC litakuwa shirika lenye mtaji mkubwa kuliko shirika lolote nchini. Aidha, aliwahakikishia Watanzania kuwa na uhakika wa huduma na ulipaji wa madai kwa muda mfupi zaidi.

Alisema kwa sasa wameweka jitihada zaidi katika utoaji wa huduma kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo itamuwezesha mteja kukata bima sehemu yoyote alipo kwa kutumia simu ya mkononi.

Pia, alisema wameendelea kufanya mabadiliko ya kiutendaji ikiwamo kuwaongezea ujuzi watendaji na kuboresha mipango ya utekelezaji wa kazi.

Alisema matarajio makubwa ni kuhakikisha huduma wanayoitoa kwa wateja inakuwa bora.

Mwenyekiti wa Bodi ya NIC, Laston Msongole, alisema NIC lilikuwa na changamoto na lilipitia wakati mgumu kwa kipindi kilichopita, lakini wamejaribu kufanya kazi na kuhakikisha kunapatikana faida.

Alisema licha ya changamoto walizopitia lakini kwa sasa NIC limekuwa likipata faida inayoongezeka kwa miaka kadhaa ikiwamo mwaka 2018 lilipata faida ya Sh.bilioni 3.62, Sh.bilioni 7.79 (2019) Sh.bilioni 33.65 (2020) na Sh.bilioni 73.10 (2021).

Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto, alisema alishiriki katika mkutano wa mwaka wa NIC ili kujua matokeo ya utendaji kazi wa shirika, kwamba alikuta mabadiliko makubwa ya kiutendaji kuliko miaka iliyopita.

Alisema: "Nilichokikuta kinatia moyo. Shirika letu limebadilika sana, sasa hivi utendaji wake umekuwa ni mzuri, unathibitishwa na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)"

## Spika Z'bar aifagilia Exim kwa kufuturisha

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, ameishukuru Benki ya Exim kwa kuandaa futari kwa wateja wake visiwani humo.

Futari hiyo iliandaliwa kwa ajili ya kuadhimisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, kwa wateja wake visiwani humo.

Hafla ya futari hiyo ilifanyika Hotel Verde visiwani Zanzibar ikihudhuriwa na wadau mbalimbali wa benki hiyo wakiwamo wateja, wafanyakazi wa benki hiyo na viongozi mbalimbali wa vyama na serikali wakiongozwa na Spika Zubeir.

Spika Zubeir aliishukuru benki hiyo kwa kuwa karibu zaidi na wateja wake kwa kutambua na kuheshimu imani zao, hivyo kuamua kuonesha kwa vitendo heshima hiyo.

"Hatua hii inaleta faraja kubwa kiimani miongoni mwa wateja wenu na hivyo wateja wanajiona kuwa sehemu salama za si tu kibiashara bali kiimani kwa hili nawapongeza sana Benki ya Exim," alisema.

Akiwaasa waislamu katika kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, Spika Zubeir alisema ni vyema walio na uwezo kuwafuturisha wasio na uwezo ili kujiongezea thawabu.

Ofisa Mkuu Idara ya Fedha Benki ya Exim, Shani Kinswaga, alisema benki hiyo imekuwa na utaratibu wa kutumia Mwezi Mtukufu wa Ramadhan kufuturu pamoja na wateja wake katika mikoa mbalimbali ili tu kuwatakia heri ya mfungo pamoja na kutoa shukrani na kuomba ushirikiano endelevu katika utoaji wa huduma za benki hiyo.

"Katika miaka yote ya utekelezaji wa shughuli zetu, Zanzibar imeendelea kuwa sehemu ya kimkakati kibiashara na tunaahidi kuendelea kushirikiana vema zaidi na wateja pamoja na Mamlaka mbalimbali za kiserikali na kidini katika kustawisha zaidi mahusiano yetu."

Kinswaga alisema benki hiyo imeshatoa mikopo mbalimbali yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 30 kwa wateja wanaohudumu sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya utalii.

"Pamoja na kufanya yote haya faraja kubwa kwetu imebaki kuwa ni ule mrejesho chanya tunaoupata kutoka kwa wateja wetu wanaotutambua kama benki yenye ubunifu na ubora. Hizi ni sifa ambazo tusingeweza kufikia bila uaminifu kutoka kwa wateja wetu...tunashukuru sana na tunaahidi kutowaangusha," alisema.




Ofisa Mkuu Idara ya Fedha ya Benki ya Exim, Shani Kinswaga, akizungumza na wageni waliohudhulia hafla ya futari iliyoandaliwa na benki hiyo, kwa ajili ya wateja wake visiwani Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Hospitali mbili zaongezewa nguvu mapambano dhidi ya UVIKO-19

**Na Mwandishi Wetu,**
MUSOMA

MIGODI ya Barrick ya North Mara na Bulyanhulu imetoa msaada wa vipimo vya kisasa vya utambuzi wa magonjwa katika hospitali mbili za mikoa.

Msaada huo ni sehemu ya mpango wa kusaidia nchi katika kupambana na kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19 na magonjwa mengine ya kuambukiza.

Katika hafla ya kukabidhi msaada huo katika Hospitali ya Rufani ya Musoma, Meneja Mkuu wa Mgodi wa North Mara ,

Apolinary Lyambiko, alikabidhi msaada huo kwa Mkuu wa Mkoa wa Mara, Ally Happi, vifaa vya kisasa vya kupima magonjwa ya kuambukiza kama virusi vya UVIKO-19, kifua kikuu, nimonia, mafua makali na magonjwa mengineyo.

Daktari mkazi katika mgodi wa North Mara, Dk. Nicholas Mboya, alibainisha kuwa utambuzi unaweza kufanywa kupitia aina mbalimbali za sampuli, kwa kuchukua vipimo kwenye pua, koo, mate au makohozi, na kutoa majibu kati ya dakika 49 na 80.

Alisema upimaji huu unadhihirisha ubora wa vipimo hivyo vya kisasa ambavyo vinaweza kutambua majibu ya sampuli nne kwa wakati mmoja.

"Tunajivunia kutoa vifaa hivi maalum ili kuimarisha miundombinu ya matibabu katika jamii zinazozunguka migodi ya kampuni," alisema Lyambiko.

# Mwongozo uzalishaji wa parachini mbioni

SERIKALI inatarajia kuzindua mwongozo wa uzalishaji wa zao la parachichi ili kuwapo na usimamizi bora wa zao hilo.

Sambamba na hilo, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) katika mwaka wa fedha 2022/23, inatarajia kuanza uzalishaji wa miche ya parachichi milioni 20 ambayo itauzwa kwa bei ya ruzuku ya chini ya Sh. 2,000.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Shally Raymond.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji Serikali ina mpango gani wa kuzalisha mbegu bora za parachichi aina ya Hass na kuwagawia wakulima kwa bei nafuu.

Akijibu swali hilo, Mavunde alisema mpango huo unalenga kuwasaidia wakulima kuanzia huduma za ugani ili kuzalisha kwa tija na serikali itaendelea kulipa kipaumbele.

Aidha, alikiri kuwa miche ya parachichi katika baadhi ya maeneo imekuwa ikiuzwa kwa bei kati ya Sh. 5,000 hadi Sh. 6,000 ambapo baadhi ya wananchi wanashindwa kumudu.

"Kwani ekari moja inahitaji miche sio chini ya 70 na kwa ekari 10 utahitaji Sh. Milioni 3.5 kwa ajili ya miche tu iwapo bei ya mche ni Sh. 5,000,"alisema.

Aidha, alisema katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali kupitia TARI inatarajia kuanza uzalishaji wa miche ya parachichi milioni 20 itauzwa kwa bei ya ruzuku ya chini ya Sh. 2,000. "Katika kudhibiti ubora wa wazalishaji binafsi, Serikali kupitia Taasisi ya Uthibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI) imeanza usajili wa wazalishaji wa miche ya parachichi nchini,"alisema.

Katika swali lake la nyongeza, Mbunge huyo alihoji serikali imejiunganishaje na wadau ili kuwa na soko la uhakika la zao hilo ikiwamo nje ya nchi.

Mavunde akijibu swali hilo, alisema hivi sasa Parachichi inauzwa India, Afrika Kusini na wanakamilisha mazungumzo na China ili kuanza kuuza huko.

"Wazalishaji wetu wadogo wamepata masoko Marekani, kuhusu masoko soko la uhakika lipo isipokuwa kulikuwa na tatizo moja kuhusu kukidhi ubora wa kimataifa hivi sasa kuna Maabara yetu Arusha tumeboresha na tumepata ithibati yenye namba 170-25," alisema.



Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa, akizungumza wakati akiliomba Bunge kujadili tangazo la zuio la bodaboda na bajaji, kuingia maeneo ya katikati ya Jiji la Dar es Salam, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Kituo cha afya Mbozi kupewa kipaumbele kwa ajira mwaka huu

Bunge limeelezwa kuwa katika ajira za watumishi wa kada za afya 7,612 zilizotangazwa wiki hii, Kituo cha Afya Itaka kitapewa kipaumbele.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa (TAMISEMI), Dk.Festo Dugange alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Juliana Shonza.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji Serikali ina mpango gani wa kupeleka Watumishi wa afya wa kutosha katika Kituo cha Afya Itaka.

Akijibu swali hilo, Dk.Dugange alisema Serikali imeendelea kuajiri na kuwapeleka watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini.

Alisema katika ajira za mwaka 2020/21 Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ilipelekewa watumishi 17 na kati yao watumishi wawili walipelekwa Kituo cha Afya Itaka.

Katika swali lake la nyongeza, Mbunge huyo alihoji mpango wa serikali wa kuwa na Daktari wa upasuaji katika kituo hicho kinachohudumia kata tano.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema serikali imepeleka fedha kwa ajili ya kujenga jengo la upasuaji kwenye kituo hicho na kwamba baada ya jengo kukamilika atapelekwa daktari wa kutoa huduma hiyo.

Pia, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Minza Mjika alihoji lini serikali itapeleka watumishi wa kutosha katika Wilaya tatu za Mkoa wa Simiyu zenye upungufu mkubwa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema mpango wa serikali ni kuendelea kuajiri watumishi kwa awamu na Wilaya hizo zitapewa kipaumbele.




Habari zote na Augusta Njoji

## Mbunge ataka majengo ya Wizara ya Elimu sasa kujengwa Zanzibar

Mbunge wa Chumbuni (CCM), Ussi Salum Pondeza, ametaka Serikali kujenga majengo ya Wizara ya Elimu Zanzibar ili wanafunzi wa elimu ya juu wapate huduma kwa wakati na kupunguza gharama za kukodi ofisi.

Akijibu swali hilo bungeni jana, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, alisema Zanzibar kuna Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yenye majengo yake ambayo ina Idara ya Elimu ya Juu inayoongozwa na Mkurugenzi kwa lengo la kuhakikisha kuwa wanafunzi wa elimu ya juu wanapata huduma.

Vilevile, alisema zipo taasisi za elimu ya Juu zinazotoa huduma kwa wanafunzi kama vile Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Karume, Taasisi ya Sayansi ya Bahari (IMS) na Tume ya Taifa Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

Alisema Serikali imeendelea kujenga ofisi katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kusogeza huduma za elimu karibu na wananchi kulingana na upatikanaji wa fedha.

"Nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa kila Taasisi ya Umma inakuwa na majengo yake kwa lengo la kupunguza gharama za kukodi ofisi,"alisema.




Madaraja ya Dar ni vyema sasa yahamie vijijini

BUFE

IJUMAA APRILI 22, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## Bodi Mkonge 'yashikia bango' uchakataji malighafi ikizipa haki Amcos kuanza kazi

Ukurasa 12

NEEMA TOKA VITA VYA RUSSIA VS UKRAINE ...

# Italia yaingia mkataba mteja wa gesi inayozalishwa Angola

- Kwingineko Afrika kwajipanga kwa neema

**Na Christina Mwakangale**



Viongozi wa nchi mbili, Italia na Angola, wakizungumza mara baada ya kuingia makubaliano kuhusu kuuziana gesi. **PICHA: MTANDAO**

TANGU Februari mwaka huu, mgogoro kati ya Russia na Ukraine uanze, suala la soko la nishati ikiwamo gesi imekuwa ikihofiwa kati ya bidhaa inayoweza kuathiriwa .

Hiyo ni kutokana na Russia kuwa msambazaji mkuu wa nishati hiyo Ulaya inayokaribia asilimia 40, inayopatikana kutoka chanzo chake, Mashariki mwa nchi hiyo.

Italia rasmi imevunja ukimya wa 'nitapata wapi gesi' baada kutia saini mkataba wa utekelezaji wa usambazaji gesi, ikisema inajitenga na gesi ya Russia yenye mgogoro.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Italia, Luigi Di Maio ametangaza hayo jana jijini Luanda, Angola, akisema wamefikia makubaliano, pia mengine muhimu anafafanua:"Nia ya dhati ya Italia ya kutofautisha vyanzo vya usambazaji wa nishati imethibitishwa."

Waziri Mkuu Mario Draghi, anasema wanaiongeza Angola na Congo-Brazzaville kwenye mpango wa wasambazaji, kuchukua nafasi ya Russia inayotoa takribani asilimia 45 ya gesi Italia.

"Hatutaki kutegemea tena gesi ya Russia, kwa sababu utegemezi wa kiuchumi haupaswi kuwa utii wa kisiasa," anasema Draghi.

Barani Afrika kuna maeneo yenye vyanzo vya nishati hiyo, petroli na dizeli, lakini teknolojia na miundombinuni ni kati ya vikwazo vinavyorudisha nyuma maendeleo.

Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz, Wakati anafafanua mgogoro wa Russia na Ukraine ukifikia takribani siku 60, huku Russia ikiwekewa vikwazo, Ujerumani ilitangaza ipo tayari kununua mafuta na gesi soko la dunia, ikiwamo Afrika, bila kuitegemea Russia.

Ujerumani ilishasitisha kuidhinishwa mradi wa bomba la 'Nord Stream 2' kutokana na Russia kuivamia Ukraine. Hilo ni bomba linaloanzia Magharibi wa Siberia hadi Ujerumani, unaogharimu Dola za Marekani bilioni 11 (Sh. trilioni 2.3), ufadhili wake ukigawanyika kati ya kampuni ya nishati za Russia na nchi za Magharibi.

Ujerumani ilitangaza kusitisha mchakato wa kutoa leseni ya bomba kati yake na Russia, uendeshaji kusimamishwa ni hatua kubwa kwa kuwa Russia inaipatia Ulaya karibu asilimia 40 ya gesi yake, inayopatikana Mashariki mwa Russia.

Ulaya inatajwa kwamba imekuwa ikitegemea kwa theluthi moja ya gesi na mafuta kutoka Russia. Wakati mgogoro unaendelea, bei ya gesi inatajwa kupaa zaidi Ulaya na kuna wasiwasi Russia itawasitishia usambazaji kabisa.

Awali nchi za Ulaya na Afrika zimeshuhudia kupanda bei ya mafuta. Inaelezwa, tayari Marekani inafanya mazungumzo na Qatar kuangalia uwezekano wa kuisambazia gesi na Umoja wa Ulaya (EU), kama mbadala wa Russia.

Ingawa kwenye jukwaa lililohusu nchi wasafarishaji wa gesi nchini Qatar Machi mwaka huu, Qatar ilisema itakuwa vigumu kwao kufikia usambazaji wa kiwango cha Russia, kwani kunahitajika uwekezaji wa miundombinu kujihakikishia utoaji huduma hiyo kwa ufanisi kuziba pengo.

Nchi za Afrika ambazo baadhi yake zina kiwango cha juu cha hifadhi ya gesi, zinajipanga kutumia fursa na kuziba pengo hilo. Mahitaji yaliyopo ni mita za ujazo bilioni 150 hadi 190 kwa mwaka, kiasi ambacho Russia imekuwa ikiisambazia Ulaya.

Nchi za Afrika zinazotajwa kuwa na nishati hiyo imo Tanzania, ingawa mzalishaji mkubwa ni Nigeria, Naibu Waziri wake wa Petroli, Timipre Sylva, akilifafanua hili kuwa: "Tunatarajia kujenga bomba 'Trans-Sahara pipeline', ambalo litasafirisha gesi hadi Algeria, kisha Ulaya,"

Nigeria inasema mazungumzo ya awali na Algeria ni kwamba ujenzi wa bomba hilo la Trans-Saharan Gas Pipeline, litakuwa na urefu wa kilomita 614, ambayo ni gesi asilia.

**SHIDA MIUNDOMBINU**

Wataalamu wa uchumi wanataja vikwazo vya miundombinu ni tatizo. Inaelezwa mradi wa Maghreb-Europe Gas Pipeline wa Algeria, ambao ndio mkubwa zaidi Afrika, ni wa gesi asilia na linasafirisha kupitia Morocco, Hispania hadi Ureno.

Ingawa nchi za Afrika zina hifadhi kubwa ya gesi, bado kuna shida ya miundombinu duni na kuvutia uwekezaji na kusambaza soko la Ulaya.

Mwaka 2020 Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari anasema, nchi yake itaweka kipaumbele kwenye gesi, ujenzi wa bomba lenye kilomita 614 (Ajaokuta-Kaduna-Kano Natural Gas Pipeline). Kiwango kikubwa cha mradi utafadhiliwa na mkopo wa benki za China.

Msumbiji, pia inatajwa kuwa na hifadhi ya gesi ikiwa ni asilimia moja ya jumla ya hifadhi yote ya nishati hiyo duniani.

Ingawa mgogoro wa Cabo Delgado mradi wa gesi wa Dola bilioni 50 (Sh. trilioni 115), eneo lenye utajiri wa nishati hiyo, unasababisha kuchelewa kupatikana kwa matunda ya thamani ya bidhaa hiyo.

Hata Nigeria nako uzalishaji mafuta na gesi unaathiriwa na usalama mdogo kutoka vikundi vya kigaidi

BIASHARA

IKIDAI WALIOPEWA TENDA WAMESUASUA...

# Bodi Mkonge 'yashikia bango' uchakataji malighafi ikizipa haki Amcos kuanza kazi

Na Hamida Kamchalla, TANGA.

- Imeteta na benki, zimewashiwa taa za kijani
- Tabasamu wakulima, baada kilio cha hasara
- Naibu Waziri: Nasi twaja na mashine uhakika

UNAPOTAJWA wasifu wa mkoa wa Tanga kiuchumi , hapana shaka wasifu unaangukia kwenye zao la mkonge na dhana hiyo inapoingia katika mustakabali mpana zaidi, umenufaisha picha pana ya taifa kihistoria.

Umma ulisafiri kutoka mikoa ya mbali, kuwinda kuajiriwa na kuna watu kutoka hata katika nchi jirani kama vile Msumbiji nao walipatikana huko, mbali na wenyeji wa mikoa mbalimbali, ikiwamo Kigoma na Rukwa.

Kuna wakati ilitokea mageuzi ya malighafi mkonge na hasa katika soko la kimataifa, iliyoendana na mageuzi ya kiteknolojia, yaliyosababisha hitaji la malighafi mkopange kushuka, kabla ya kuanza kuhitajika tena hivi sasa na nafasi yake kuanza kurudi kwa kasi.

Mbali na Tanga, pia mikoa kama Morogoro imekuwa juu katika uzalishaji mkonge, zao linalosimamiwa na chombo maalum, Bodi ya Mkonge Tanzania.

Sasa inatangaza imenuia kupandisha takwimu za uzalishaji wa zao hilo kwa kuruhusu vyama vya Ushirika (Amcos) wilayani Korogwe, mkoa wa Tanga kufunga mashine za kuchakata (korona) mahali ziliko.

Mkonge ukiwa katika orodha ya mazao ya kimkakati, hadi sasa takwimu zake zilizopo inaelezwa ziko chini zaidi kufikia malengo yaliyopo kitaifa. Hivyo, bodi hiyo sasa inatafuta mbinu mbadala kupandisha kiwango cha uzalishaji kufika tani 120,000 ifikapo mwaka 2025.

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Mkonge nchini Saad Kambona, anaeleza tangu serikali ilipoamua kulirudisha chini yake kutoka katika kampuni ya Katani Limted, ikiwa ni zao la kimkakati, hali ya kusuasua uzalishaji imeonekana.

Anaeleza ni hatua ambayo serikali itasimamia zao hilo, ikiwa na usaidizi wa kampuni mpya ya kuchakatia mkonge, kutoka ile ya awali NSSF, kukishuhudiwa huduma za uchakataji kuzidi kuzorota.

"Mkonge mwingi wa wakulima unabaki shambani bila ya kuvunwa kwa wakati na hiyo ni hasara kubwa kwa wakulima hao, pia kwa taifa kwa sababu takwimu zetu za uzalishaji zinazidi kushuka," anasema.

Kambona anashauri:"Tunapaswa kuelekea kwenye uzalishaji wa tani 120,000, kasi yetu ya kuelekea kwenye kutimiza hilo lengo la serikali haiendi kwa kiwango kile tunachotaka, kwa sababu eneo la uchakataji haliko vizuri.



Shughuli zikiendelea ndani ya kiwanda cha uchakataji mkonge. **PICHA: MTANDAO.**

**"Niwaondoe hofu wakulima na tutafanya kazi hii kwa pamoja kwa kushirikiana na watu wa mazingira (NEMC), ili agizo la Waziri Mkuu litekelezwe kwa uharaka zaidi.**

"Kwa hiyo tukasema tunaruhusu 'Amcos' ziwe na makorona yao zenyewe, ili kuongeza ushindani kwenye eneo la uchakataji na kuhakikisha kwamba mkonge wote unaostahili kuchakatwa unachakatwa mara mbili kwa mwaka, jambo ambalo hivi sasa halifanyiki" anasisitiza.

**BODI NA BENKI ZATETA**

Kutokana na hilo, anasema Bodi ya Mkonge imefanya maongezi na benki kuziwezesha Amcos zote tano kwa kuwakopesha korona, ambazo watazimiliki na tayari benki zimeshakubali.

Pia, anasema tayari bodi imeshawapatia wahusika maeneo ya kufunga mitambo ya kuendeshea korona hizo. Anafafanua:"Benki za CRDB na NMB zimekuwa na mazungumzo na hizi Amcos na zimeonyesha hazina shaka yoyote kuhusu kuzikopesha.



Mkonge uliovunwa tayari kupelekwa kiwandani kuchakatwa. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

"Tunasubiri mchakato ukamilike wa maandiko ya mradi, kupima udongo pamoja na NEMC zikikamilika tu, benki zitakopesha Amcos zetu.

"Pia, tumetoa maeneo kwa Amcos kwenye mashamba ya Magunga, Mwelya, Mgombezi, Magoma na Hale kwa ajili ya kuweka miundombinu yao ya makorona, wafunge na waanze kuchakata, tunaamini kwa kufanya hivi, uzalishaji wa mkonge utaongezeka kwa haraka sana" anasema Kambona.

**VIONGOZI USHIRIKA**

Wenyeviti wa Amcos wa Korogwe, wanasema kuna kero nyingi kwa nyakati tofauti zinazowakabili wakulima wa mkonge wa wilaya za Korogwe, mkoani Tanga zinazosababisha hasara kubwa kwa wakulima, hali inayowafanya wakulima kukata tamaa ya kuendelea na kilimo hicho.

Mwenyekiti wa Hale Sisal Amcos, Yusuph Nkondo, anaainisha kero hizo ni ubovu wa mitambo ya uzalishaji, gharama kubwa za usindikaji, kufanya kazi nje ya mkataba na ubovu wa barabara wanazopita kwenye mashamba ya mkonge.

Nkondo anasema kwamba mitambo hiyo imekuwa ikiharibika kila mara na kusababisha mikonge ya wakulima kuharibika, hali inayowashushia madaraja, jambo linalompunguzia pato mkulima na kuleta hasara.

"Kuharibika mitambo kunawachelewesha wakulima kuvuna mkonge wao kwa wakati na kusababisha kukauka mashambani. Hii ni hasara kubwa sana kwa wakulima, kwani pesa ambayo wamewekeza hairudi" anasema Nkondo, anayeendelea:

"Kutokana na gharama ya usindikaji kuwa kubwa, imekuwa ni mzigo mzito sana kwa wakulima wetu ambayo imekuwa inapunguza sana kipato chao, pamoja na ari ya mkulima kulipenda zao la mkonge.

"Kwani wanaona ni kama pesa yote anayotegemea kuipata inaishia kwa msindikaji ambaye anachukua pesa nyingi bila kujali ubora wa singa zinazozalishwa".

Anafafanua kuwa vyama vya ushirika hadi sasa vinafanya kazi zake hizo nje ya mkataba na kampuni yenye dhamana ya kuchakata mkonge kwa sasa, hali inayofanya Amcos zote tano za wilayani Korogwe, kuwasilisha pendekezo serikalini la kushuka bei ya usindikaji.

"Iliundwa kamati maalumu kufuatilia hilo, upangaji wa bei na baada ya kamati kumaliza na kuleta mapendekezo yake, hadi sasa bado tupo kwenye hali ya sintofahamu kwani hatujui ni kitu gani kimekwamisha.

"Tumekuwa na changamoto ya barabara mbovu ambazo pia zinachangia kuchelewesha uvunaji mkonge kwa wakati, pia kipindi cha mvua zinakuwa hazipitiki na kusababisha kupunguza uvunaji".

**JICHO LA WAKULIMA**

Wakulima wa mkonge wanasema wamekuwa wakipata hasara kubwa kwa mazao yao kushindwa kuchakatwa, sasa wanapiga kelele kuitaka bodi kuwezesha kila Amcos kumiliki korona lake, ili waweze kupata wanachokitafuta, kwani wamepewa matumaini na serikali kwenye zao hilo, kuwafufulia ari waliokata tamaa.

Malalamiko yao yanaangukia namna mkonge wao unavyoharibika shambani, kisha mchakataji anatoa sababu nyingi hasa za mashine zimeharibika.

Aidha, eneo lingine wanalolamikia ni kuwapo bei kubwa ya uchakataji mkonge kwa kiasi ambacho kinawafanya wasibaki na pesa kubwa, baada ya kupatiwa 'advansi' za kuandaa mashamba hadi hatua uvunaji.

Hata hivyo, wanarejesha shukrani kwa Bodi ya Mkonge, kufikia hatua ya kukubali ombi lao wakulima, Amcos kuwezeshwa kumiliki makorona ya uzalishaji kusaka ngazi ya malengo ya serikali kuzalisha tani 120,000.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO**

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, anasema uchakavu wa mitambo ni tatizo kubwa linalofifisha ubora wa mkonge, kupotea kwake, hata kuangukia ujumla wa hasara, athari inayomuangukia mkulima ambaye amefuata kanuni zote za ubora alizopewa.

Mavunde anasema, serikali imenuia kulifufua zao hilo, pia kuhakikisha inawawezesha wakulima kuwa na manufaa yatakayowafanya waishi na kuendeleza kipato chao na Taifa kwa ujumla, ili waone thamani ya kilimo wanachofanya.

"Tayari bodi imeshatangaza zabuni ya ununuzi wa korona kubwa tatu, ambazo zitasaidia kuufanya mkonge wetu ambao umekuwa ukikauka mashambani kutowepo, pia mkulima kuvuna mkonge wake mara mbili kila mwaka.

"Nimeshamuagiza Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Mkonge kufanya mara moja mchakato wa kuanza kutoa tangazo la zabuni kununua makorona mengine matatu kwa ajili ya kusaidia uchakataji zao la mkonge, ili tuwe tumemrahisishia mkulima kupata sehemu ya uhakika ya kuchakatia mazao yao" anafafanua.

Mavunde anaahidi serikali itahakikisha inapata masoko ya uhakika ya mkonge wa nchini, ili kuchochea kilimo chake, karika mkoa wa Tanga na mingine 17 inayojihusha na kilimo hicho.

Pia, anakiagiza kiwanda cha kuchakatia mkonge binafsi kilichopo kufanya uwekezaji mkubwa, kwani bado wana mashine ambazo hazifanyi kazi.

"Niwaondoe hofu wakulima na tutafanya kazi hii kwa pamoja kwa kushirikiana na watu wa mazingira (NEMC), ili agizo la Waziri Mkuu litekelezwe kwa uharaka zaidi.

"Watu wengi sana wamepata ajira kupitia kiwanda chenu, pia zao la mkonge, tutafanya hivyo pia kwa ajili ya kuhakikisha tunakuza uchumi wa kaya, lakini na uchumi wa mtu mmoja mmoja.

"Nitoe rai kwa maeneo yote wanayolima mkonge nchini muendelee kuiamini bodi yetu na mjitokeze kwa wingi sana katika kilimo hiki. Najua mlikuwa mna tatizo la mkonge wenu kubaki shambani kutokana na kutokuwepo makorona mengi ya kuchakatia, " anaeleza.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Madaraja ya Dar es Salaam ni vyema sasa yahamie vijijini




NAPENDA sana kuangalia makala za wanyama kwenye televisheni, hasa zile zinazohusu wanyama na hasa kwa kuwa Tanzania tuna utajiri huo wa maliasili, hujivuna sana ninapowaona mbugani na hifadhini.

Lakini, huvutiwa sana ninapoona wale nyumbu wahamao kutoka Tanzania kwenda Kenya. Hunifurahisha kutokana na ujinga wao wa kufuatana bila kuachana na hata mmoja anaponaswa na mamba, mwingine hupita hapo hapo na kukamatwa.

Kwa binadamu nao na ni ujinga, lakini pengine kwao nyumbu wanadhani ni ujanja, na utamwona anaangalia mwenzake akizamishwa huku akilia, lakini naye atajipeleka hapo hapo na kunaswa.

Nyumbu hukosa ushirikiano sana wanaposhambuliwa hata na simba, chui au duma, ni tofauti na mbogo ambao wanapokuwa wengi na wakamwona mwenzao amenaswa, hufuatilia na kukabiliana na adui hata kumwokoa.

Nasema hufurahia sana kushuhudia ujinga wa nyumbu, lakini huniuma sana nisikiapo au kuona binadamu kapita mtoni na kukamatwa na mamba na kupoteza maisha au kujeruhiwa na kupata ulemavu wa maisha.

Taarifa za watu kukamatwa na mamba zipo sana nchini na zinaonyeshwa pia kwenye televisheni, kama zioneshwavyo za nyumbu wahamao Serengeti kwenda Maasai Mara, Kenya kupata mimba na kurudi kuzaliana nchini.

Inauma sana kuona binadamu mwenzio anakamatwa na mnyama na wewe huna jinsi ya kuzuia, lakini una namna ya kuepuka kadhia hiyo na kupunguza matukio hayo kama si kukomesha kabisa.



NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com.

Matukio kama hayo na ambayo mengine yameripotiwa hivi karibuni, ni pale wanakijiji fulani wanaoishi kando ya mto wanapotaka kuvuka kwenda upande wa pili kufuata mahitaji au huduma, hulazimika kupita mtoni.

Kibaya zaidi ni kwamba, mto husika hauna daraja, hivyo hujitosa majini na kupita ama kwa kutembea au wengine kwa kuogelea. Lakini, katika mto husika kuna mamba wa kutosha wenye njaa na ambao huvizia riziki kwa kila avukaye.

Katika kijiji kimoja kuna watu wamepoteza maisha na baadhi kukatika miguu au mikono na kubaki na ulemavu wa kudumu, hiyo ni kwa sababu hakuna madaraja.

Wakiulizwa wananchi wanajibu walishakuja viongozi na wataalamu na kupima na kuahidiwa kujengewa madaraja, lakini ni miaka sasa tangu waondoke, hawajarudi wala kurudisha salamu tu kwamba lini watakuja kutekeleza.

Watasema hata bungeni wamekuwa wakisikia ahadi zikitolewa kupitia majibu ya maswali na hata makadirio ya wizara, kuwa daraja la mto fulani litajengwa katika bajeti ya mwaka huu wa fedha, lakini wapi, niliko mbioni au mchakato unaendelea.

Unajiuliza, hivi Watanzania hawa masikini wataendelea kutafunwa na mamba mpaka lini? Hivi masikini hawa wataendelea kupewa mgawo wa ulemavu mpaka lini, wakati wana viongozi wao na huku pia wanaendelea kulipa kodi kama kawaida?

Hivi tujiulize Watanzania hasa mnaoishi Dar es Salaam kuna haja ya kuendelea kujenga madaraja ya mabilioni ya fedha nchi kavu mijini, huku wananchi vijijini wakiwindwa na mamba kwa sababu tu ya kuvuka mito kutafuta mahitaji na huduma?

Madaraja tukiambiwa yanapunguza foleni Dar es Salaam, hivi hilo limejiri kweli? Mtokao Ubungo kwenda Bandari ya Dar es Salaam na kurudi mnaweza kushuhudia.

Sasa tunajenga mengine kwenye makutano ya Chang'ombe, tunajenga na lingine pale makutano ya barabara za Mandela na Kilwa. Tunapanga kujenga mengine na mengine, katika makutano mengine.

Ni mtazamo, hatuwezi kuyaahirisha hayo hasa katika jiji hili ambalo watu wamehamia Dodoma, tukaangalia kwanza wananchi wetu vijijini yanayowasibu tukayatatua kwanza ndipo turejee kuyajenga haya kama yana uzito na umuhimu kweli?

Natafakuri tu hivi hatuwezi kuwa na madaraja katika mito mingi yenye mamba na kunusuru maisha ya Watanzania wenzetu wasiojua kama kesho litachomoza?

Chukua gharama za madaraja makubwa ya Dar es Salaam, ulinganishe na vijidaraja vinavyotakiwa vijijini kama hatutaweza kufanya hayo.

Kwanza havina gharama ni vi-milioni kadhaa tu hivi. Nitashangaa kusikia bajeti ya ujenzi mwaka huu ina madaraja ya Dar es Salaam. Alamsiki.

UCHUMI

# Simulizi za LHRC, Uviko -19 ulivyokwaza uchumi kupaa

## • Kasi ya ukuaji wake ulibadilika ghafla




Rais Samia Suluhu Hassan, mwaka jana alipozindua kampeni kuikabili Uviko - 19 kitaifa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Christina Mwakangale**

JUZI Jumanne, gazeti hili lilichapisha maudhui ya Ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, ikieleza mustakabali namna maradhi Uviko - 19 ulivyozua vikwazo katika nyendo za kisiasa kitaifa. Endelea kufuatilia kinachojiri katika uchumi:

WIKI iliyopita Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kilizindua Ripoti ya Haki za Binadamu 2021 jijini Dar es Salaam, inayotolewa kila mwaka, ikilenga mambo kadhaa kwenye jamii iliko na iendako, hata ikatoa mustakabali wake.

Ni mtazamo unaoangukia dhana ya maendeleo ambayo mwanazuoni, Prof. Walter Rodney, anaitafsiri kwamba ni mabadiliko ya idadi ya vitu kuongezeka, pia hali yake kuelekea kwenye ubora zaidi.

Mathalan, mtu anapokuwa na idadi zaidi ya vyakula, pia ubora maradufu kukidhi mahitaji yake, hapo anakuwa amepata maendeleo ya chakula.

Umoja wa Mataifa (UN) unayafafanua maendeleo, kwamba ni haki ya binadamu isiyoondolewa kwa nguvu ambayo kila mtu na watu wote wana haki ya kushiriki, kuchangia na kufurahia maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa.

Ripoti zinazijikita kwenye masuala ya haki za binadamu, ikiwamo kuu ya kuishi kiuchumi, kielimu, kijamii, kisiasa na mwaka uliopo unaitaja Uviko-19, ulichangia kushusha uchumi wa mtu mmoja mmoja hadi kitaifa.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba.

Akizindua ripoti hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, anataja Uviko-19 imo katika orodha ya yaliyokwamisha uchumi nchini, hata kushusha kiwango cha haki ya kiuchumi ndani ya wanajamii.

Ripoti inaitaja Uviko-19 ilikuwa na athari kubwa katika kutambua haki za binadamu mwaka jana, hasa penye haki za kijamii na kiuchumi, akisema kwa ujumla wanawake na watoto ndio waliathirika zaidi.

"Kama ilivyokuwa kwa haki zingine za binadamu, janga la Uviko-19 halikuacha haki za kijamii na kiuchumi. Wanajamii walijibu Utafiti wa Haki za Kibinadamu 2021 walioulizwa jinsi janga hilo lilivyoathiri haki zao za kiuchumi na kijamii," anasema.

Ripoti mwaka huu inafafanua kwamba, mwaka juzi, Tanzania ilipiga hatua kubwa, hasa katika ukuaji uchumi wake kutoka nchi zenye kipato cha chini hadi kipato cha kati. Hata hivyo, anataja Uviko-19 ilipunguza kasio ya ukuaji huo wa uchumi kama ilivyokuwa katika nchi nyingine nyingi.

Anasema, ukuaji Pato la Taifa (GDP) uliripotiwa kushuka kutoka asilimia 7.0 mwaka 2019 hadi 4.8 mwaka 2020, huku sekta muhimu kama vile utalii na viwanda zikiathiriwa sana na janga hilo na kuathiri ukuaji uchumi kitaifa.

"Kupoteza au kupunguza mapato ambayo ni asilimia 93, kulitajwa kuwa ni athari ya Uviko-19, ikifuatiwa na mabadiliko ya vyanzo vya mapato (86%), usumbufu wa elimu (82%) na ufikiaji mdogo wa huduma za afya (81%).

"Madhara mengine ya janga hili kwa haki za kijamii na kiuchumi ni pamoja na kuzorota kwa afya ya akili (76%), uhaba wa chakula (72%) na kupoteza ajira na kazi (71%)," anaeleza Anna, anayenukuu maudhui ya ripoti hiyo.

Pia, kiserikali analitaja janga Uviko-19 lilitatiza kwa kiasi kikubwa utoaji huduma za kijamii, hasa katika sekta za elimu na afya ambayo watumishi wale walielemewa na majukumu maradufu, ilhali hata kabla walikuwa na upungufu wa watumishi.

Lingine la madhara analolitaja kutoka mkasa wa Covid -19, ni kwamba sekta utalii imepoteza mapato kwa kiasi kikubwa, hata kuwa changamoto kubwa kwa serikali.

**BIASHARA & HAKI BINADAMU**

Hapo anarejea Ripoti ya Haki za Binadamu na Biashara ya Mwaka 2020/21 iliyoandaliwa pia na kituo hicho, ilifichua madhara kwa haki za wafanyakazi katika sekta binafsi na biashara.

Anna anataja madhara kwa wafanyakazi, ikijumuisha kutolipwa mishahara, kuchelewa kulipwa mishahara, kupunguzwa kwa mishahara, kuachishwa kazi pasipo kufuata haki, kupoteza ajira kutokana na kupunguzwa kazi, likizo isiyo na kikomo na kuongezeka kwa mzigo wa majukumu ya kazi.

Mkurugenzi Anna anataja madhara ya kibiashara yanajumuisha biashara kufungwa kwa muda, kupunguzwa uzalishaji, utumiaji gharama kubwa za huduma kibiashara, kutokana na kutumia wauzaji wengine.

Mengine anayataja kuwa ni ucheleweshaji magizo ya mizigo kutoka nje, kulipwa riba kubwa, ongezeko la kodi, kukatishwa mikataba na makubaliano, hisa kuisha, hasara za uzalishaji na katika mauzo sokoni.

Ripoti ya mwaka huu inafafanua kuwa Agosti 2021, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), ilibaini kuwa migogoro ya wafanyakazi iliongezeka kutokana na Uviko-19, ikilinganishwa na vipindi vya awali.

"Mizozo mingi ilikuwa kuhusu kusitishwa kwa ajira, huku waajiriwa wakiachishwa kazi kukabiliana na hali ya janga," anasema Anna, huku akifafanua kubainika migogoro 6,000 katika kipindi hicho cha Uviko-19. Maambukizi ya Uviko-19 barani Afrika, yanatajwa kuwa ya chini zaidi tangu kuripotiwa kwa mara ya kwanza kwenye mlipuko huo wa mwaka 2020, wagonjwa walioripotiwa wamepungua sambamba na idadi ya vifo mwaka huu.

Shirika la Afya Duniani (WHO), Kanda ya Afrika limesema hayo wiki chache zilizopita, kupitia taarifa yake iliyotolewa mjini Brazaville, Congo.

"Maambukizi kwa kiasi kikubwa yakitokana na wimbi la nne la mnyumbuliko wa virusi vya Omnicron, yamepungua kutoka wagonjwa 308,000 kwa wiki mwanzoni mwa mwaka huu hadi chini ya wagonjwa 20,000 katika wiki inayoishia Aprili Mosi, mwaka huu," inasema taarifa hiyo.

Katika wiki moja iliyopita, taarifa ilisema takribain kulikuwa na wagonjwa 18,000 na vifo 239, idadi ambayo imepungua kwa asilimia 29, ikilinganishwa na wiki iliyotangulia.

Kipindi cha muda mrefu cha idadi ndogo ya maambukizi na vifo barani Afrika kutokana na COVID-19 ilishuhudiwa tangu Agosti Mosi na Oktoba 10 mwaka 2021.

WHO inasema, kwa sasa hakuna nchi ya Afrika inayoshuhudia ongezeko la Uviko-19, huku Mkurugenzi wa WHO Kanda ya Afrika, Dk. Matshidiso Moeti anashauri ni vyema nchi zikaendelea kuwa makini na kuzingatia mikakati ya kujikinga.

"Kuwepo na utaratibu ambao unaweza kurejesha haraka mifumo ya usimamizi na udhibiti wa Covid -19, iwapo mlipuko utaibuka tena," anafafanua.





## Wakulima wanawake wataka punguzo tozo kwa vifaa umeme jua

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKULIMA wadogo wanawake wameiomba serikali kupunguza tozo kwenye vifaa vya umeme wa jua vinavyozalisha umeme kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Wametoa ombi hilo ili kuwawezesha wakulima kununua kwa bei nafuu, hivyo kuongeza uzalishaji.

Walisema hayo wakati wa kikao cha kamati ya Bunge ya kilimo, mifugo na maji kujadili Ripoti ya tatu ya Mpango wa kuendeleza kilimo Afrika ulioandaliwa na Shirika la Action Aid.

Mkulima kutoka Mbeya, Flora Mlowezi, alisema kuna haja kwa Serikali kupunguza tozo kwenye vifaa hivyo kwa ajili ya Kilimo cha umwagiliaji jambo litakalochangia wakulima kununua kwa wingi.

Mlowezi alisema pia Serikali isianzishe skimu mpya kwenye maeneo ambayo tayari yana skimu ambazo hazifanyi kazi.

"Kuna miradi mipya ya umwagiliaji ilipewa fedha ifanye ukarabati , tunaomba Serikali ifufue skimu za zamani kwanza kabla ya kuanzisha skimu mpya," alisema.

Fredina Saidi kutoka Kishapu mkoani Shinyanga, aliomba

Serikali kupunguza tozo kwenye vifaa vya umeme wa jua zinazozalisha umeme kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ili kuwezesha wakulima kununua kwa bei nafuu hali itakayowezesha kuzalisha zaidi.

Pia wakulima wanahitaji tafiti na teknolojia kwa ajili ya maendeleo yao.

Pia alisema mbegu za asili zinazotumiwa na wakulima kwa baadhi ya maeneo zinaonekana kufanya vizuri kuliko mbegu zinazotoka nje ya Nchi..

Mtendaji Mkuu wa Kilimo Hai Tanzania Bakari Mongo, alisema kilimo kinaongozwa na sera, mikakati na mipango.

"Tuko kwenye mkakati wa kutengeneza kilimo hai na ikolojia Tanzania, tuko katika utaratibu wa kutafuta maoni kwa wakulima, kilimo kiwe na sura ipi,ombi la kupata sapoti na raslimali fedha," alisema.

Mratibu wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) Mkoa wa Morogoro, Joseph Ngasenga, alisema miongoni mwa masuala yanayotakiwa kupewa kipaumbele ni upatikanaji wa mikopo kwa wakulima wadogo.

Alisema kuwa suala la sera kusisitiza Benki Kuu kutoa sheria itaelekeza taasisi za fedha kutenga asilimia 60 ya mikopo itakayotolewa kwa wazalishaji.

# Mazingira ya kazi ofisi za umma kutathminiwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, amezindua mpango maalum wa kutathmini mazingira ya kazi katika ofisi zote za serikali utakaofanyika sambamba na upimaji wa afya za wafanyakazi wote.

Mpango huo pia lengo lake ni kuwapa mafunzo stahiki ya usalama na afya mahali pa kazi.

Prof. Ndalichako akizindua mpango huo jijini Dodoma, alisema ulianza kutekelezwa kwa mwezi mmoja kuanzia Aprili 20, 2022 ambapo utahusisha mambo mbali mbali ikiwamo ukaguzi wa mifumo ya Usalama katika Ofisi za Wizara mbali mbali ikiwemo miradi ya ujenzi katika Mji wa Serikali-Mtumba.

Alisema kuwa mambo mengine ni pamoja; Uchunguzi wa afya za wafanyakazi, mafunzo ya huduma ya kwanza mahali pa kazi pamoja na mafunzo kwa wawakilishi wa kamati za usalama na afya mahali pa kazi yatakayoambatana na uundaji wa kamati husika.

"Kimsingi OSHA ina wajibu wa kulinda nguvukazi kupitia kusimamia utekelezaji wa Sheria Na. 5 ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003 pamoja na kanuni zake.

Kwa mujibu wa Sheria tajwa, OSHA inapaswa kuhakikisha kwamba inayatambua maeneo yote ya kazi nchini kwa kuyapatia usajili na kisha kuyafikia kwa ajili ya kufanya tathmini ya hali ya mazingira ya kazi, kutoa mafunzo stahiki kwa wafanyakazi pamoja na kuchunguza afya za wafanyakazi kutegemeana na shughuli wanazozifanya," alisema Prof. Ndalichako.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema mpango huo ni mwendelezo wa mkakati wa taasisi yake wa kufanya tathmini ya mazingira ya kazi nchini kisekta.

"Leo tumezindua mpango huu wa ukaguzi, mafunzo na upimaji afya kwa wafanyakazi wote wa serikali tukianza na Ofisi ya Waziri Mkuu ambapo programu hii ni mwendelezo wa makakati wetu wa kuzifikia sekta zote za uchumi kikamilifu. Lengo la zoezi hili ni kuandaa rejista ya vihatarishi vya kila sekta na hivyo kurahisisha uandaaji wa mikakati ya kukabiliana na vihatarishi hivyo katika kila sekta," alisema Khadija.

Baadhi ya wafanyakazi katika Ofisi ya Waziri Mkuu waliohudhuria hafla ya uzinduzi, walitoa maoni kuhusu mpango huo ambapo walisema utasaidia katika kuboresha mazingira yao ya kazi.

"Kwa ujumla mpango huu ni mzuri sana na utatusaidia watumishi kufanya kazi zetu kwa kuzingatia tahadhari muhimu dhidi ya vihatarishi mbali mbali.

Aidha, kupitia mpango huu ambao utahusisha tathmini ya kina ya mazingira ya kazi, itakuwa ni fursa muhimu kwa mwajiri wetu kuboresha mazingira ya kazi kutokana na mapendekezo yatakayotolewa na wataalam wa OSHA," alisema Aloyce Kirumbi ambaye ni Ofisa Utumishi katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Waziri Prof. Ndalichako katika uzinduzi wa mpango huo utatekelezwa kwa mwezi mmoja ambapo mazingira ya kazi katika Wizara zote yatafanyiwa ukaguzi na wataalam wa OSHA.

Aidha, baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, yatatolewa mapendekezo ya kitaalam ambayo yatatumika na serikali katika kuboresha mazingira ya kazi.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma juzi, kuhusu maandalizi ya maadhimisho ya sherehe za miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, zitakazofanyika kitaifa Aprili 26 mwaka huu, jijini humo. Kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mfumo kudhibiti ajira za watoto sokoni waanza

**Na Paul Mabeja,**DODOMA

KATIKA kukabiliana na ajira kwa watoto, uongozi wa soko kuu la Majengo jijini Dodoma unapanga kuandaa mfumo wa kusajili wabeba mizigo watakaopewa vitambulisho rasmi vitavyowatambulisha kwa wateja.

Pia, uongozi huo upo katika mchakato wa kusajili madalali ili kuondokana na malalamiko ya wafanyabiasahra ambao wamekuwa wakidhulumiwa mizigo yao na matapeli.

Mwenyekiti wa soko hilo, Godson Rugazama, alibainisha mpango huo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mikakati ya soko hilo pamoja na kukabilina na ajira kwa watoto.

Alisema soko hilo lipo katika hatua za kuandaa mfumo wa kusajili wabeba mizigo ambao watatambulika rasmi kwa uongozi na kupatiwa vitambulisho ili kukomesha ajira kwa watoto ndani ya soko.

"Awali tulikuwa na mfumo huu wa kusajili wabeba mizigo lakini hivi sasa umekufa tunapanga kurejesha tena ili watoto wote wanaofanya kazi ya kubeba mizigo ndani ya soko kuondolewa kabisa.

"Watu ambao watasajiliwa ni wale wenye umri unaostahili na kupatiwa vitambulisho ili wale ambao wamekuwa wakija katika soko hilo na kuzunguka ndani bila kuwa na kazi ya kufanya uongozi utawaondoa kupitia mfumo huo,"alisema Rugazama

Vilevile, alisema wana mpango wa kusajili madalali ndani ya soko ili kuondoa malalamiko ya wafanya biashara ambao wamekuwa wakitapeliwa mizigo yao.

Kadhalika alisema wafanyabiashara wa soko hilo wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo gharama za mizigo.

"Hivi sasa Soko la Ndugai limekuwa mzigo kwetu kwani jiji linatulazimisha kushusha mizigo yetu katika soko hilo na kulazimika kutumia gharama mara mbili za kusafirisha mizigo,"alisema

Waliuomba uongozi wa jiji la Dodoma kuwaondolea mzigo huo kwa kua hivi sasa unachangia katika kuwafilisi mitaji yao.





# Mgomo wa daladala watikisa kwa siku mbili

**Na Nebart Msokwa,** TUNDUMA

MGOMO wa daladala watikisa Mji wa Tunduma mkoani Songwe kwa siku ya pili mfululizo ambapo madereva wanataka nauli ziongezeke kutokana na ongezeko la bei ya mafuta na serikali imezuia mpaka utaratibu mpya utakapotolewa.

Madereva hao wamekuwa wakifanya fujo kwa kuzuia vyombo vingine vya usafiri kubeba abiria katika kipindi hiki cha mgomo jambo ambalo limesababisha serikali kuingilia kati na kutishia kuwachukulia hatua za kisheria

Jana Mkuu wa Wilaya ya Momba, Fakh Lulandala, ameagiza pikipiki za magurudumu matatu maarufu kwa jina la bajaji kuendelea kufanya kazi ya kubeba abiria kutoka Tunduma mpaka Mpemba ambako awali walikuwa hawaruhusiwi.

Lulandala aliliagiza Jeshi la Polisi wilayani humo kufuatilia na kuwachukulia hatua kali madereva daladala watakaowazuia madereva bajaji na vyombo vingine kubeba abiria.

Vilevile, aliwataka kama wanaendelea na mgomo huo yuko tayari kuagiza magari mengine yakiwamo ya serikali kuanza kubeba abiria ili kuwasaidia wananchi ambao wanashindwa kufanya shughuli zao.

"Mimi ndiye Mkuu wa Wilaya hii na hili nitalimudu, siwezi kusubiri Rais Samia au Mkuu wangu wa mkoa aje, nawatahadharisha madereva ambao wanafanya fujo waache mara moja vinginevyo nitawashughulikia," alisema Lulandala.

Hata hivyo, alisema hawezi kuruhusu nauli kupanda mpaka serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA), itakapotangaza nauli mpya.

# Mshangao meli za Ziwa Nyasa makabidhiano kufanyika Mwanza

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida, mchakato wa makabidhiano ya meli za Ziwa Nyasa kutoka Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kwenda kwa Kampuni ya Meli Tanzania (MSCL), umeanza kufanyikia mkoani Mwanza badala ya Mbeya mahali zilipo meli hizo.

Taarifa ambazo gazeti hili limeipata inaonesha maofisa wa TPA, MSCL na wengine kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, walikutana jijini Mwanza Aprili 12, mwaka huu kwa ajili ya kukamilisha hati ya makabidhiano ya meli hizo.

Hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la serikali la kuitaka Mamlaka ya Bandari kukabidhi meli zote inazozimiliki ndani ya Ziwa Nyasa kwenda kwa Kampuni ya Meli Tanzania kwa lengo la kuongeza ufanisi wa uendeshaji wa meli hizo.

Kwa niaba ya serikali, agizo hilo lilitolewa Machi Mosi, mwaka huu na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alipofanya ziara katika Bandari ya Kiwira wilayani Kyela mahali yalipo makao Makuu ya Bandari za Ziwa Nyasa.

Akiwa bandarini hapo, Naibu Waziri huyo alishuhudia meli zote tatu mpya zilizojengwa na serikali hivi karibuni kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 27 zikiwa hazifanyi kazi na zimeegeshwa bandarini hapo ikiwamo ya abiria.

Katika ziara hiyo, Naibu Waziri Mwakibete, alitoa mwezi mmoja kwa Mamlaka ya Bandari kukamilisha matengenezo ya meli ya abiria ya MV Mbeya II ili ianze kutoa huduma ya usafiri kwa wananchi wa mwambao wa Ziwa Nyansa ambao wana uhitaji wa huduma hiyo. Hata hivyo, Aprili 19, mwaka huu, Naibu Waziri Mwakibete, alirejea tena bandarini hapo kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa maelekezo yake na kushuhudia matengenezo ya meli hiyo yakiwa bado hayajaanza jambo ambalo lilionyesha kumkera.

Kutokana na hali hiyo Naibu Waziri alitoa mwezi mmoja kwa maofisa wa TPA na wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), kukamilisha matengenezo ya injini ya meli hiyo yanayogharimu zaidi ya Sh. milioni 300 huku akitishia kuwaondoa kwenye nafasi zao maofisa wanaokwamisha matengenezo hayo.

"Tunataka meli hii itengenezwe, hatutaki longolongo zenu, tuliwapa mwezi mmoja, lakini mmeishia kufanya hizo 'procurement' (manunuzi), nawapa tena mwezi mmoja na msipokamilisha tutachukua maamuzi magumu ya kuwaondoa kwenye nafasi zenu," alisema Mwakibete.

Pamoja na maagizo hayo, Naibu Waziri alipokea taarifa ya utekelezaji wa maagizo yake ya Machi mosi na iliwasilishwa na Mkurugenzi wa Huduma za Meli wa TPA, Kapteni Abdallah Mwengamno.

Kwenye taarifa hiyo ambayo Nipashe lilifanikia kupata nakala, inaonesha namna mchakato wa makabidhiano ya meli hizo kati ya TPA na MSCL ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Naibu Waziri.

Mwengamno alisema baada ya kikao cha kwanza cha mchakato wa makabidhiano kufanyika Mwanza, pia timu ya wataalamu wa TPA, MSCL na wizara, wanakusudia kufanya ukaguzi wa meli hizo Aprili 25, mwaka huu.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Loleza, wakifuatilia mafunzo ya elimu ya makuzi kwa wasichana, yaliyoandaliwa na moja ya taasisi zinazohusika na masuala ya makuzi ya vijana, jijini Mbeya, hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Baadhi ya walimu wadaiwa kufundisha mitaala ya zamani

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

BAADHI ya walimu wa masomo ya Hisabati na Sayansi wa Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, wanadaiwa kuwafundisha wanafunzi kwa kutumia mitaala ya zamani hali inayosababisha idadi kubwa ya wanafunzi kutofanya vizuri kwenye mitihani.

Hali hiyo imebainika kupitia utafiti maalumu uliofanywa na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), ambao umebaini kwamba walimu hao hawatumii mitaala mipya iliyotolewa na serikali.

Msimamizi wa Mradi wa Kuendeleza Masomo ya Hisabati na Sayansi kwa Shule za Sekondari (SMASE), Mkoa wa Mbeya, ambaye pia ni mhadhiri wa Chuo cha MUST, Dk. Leoncia Kibani, alisema hali hiyo inazorotesha elimu.

Alisema walibaini pia hali hiyo kupitia kwa walimu wanaotoka Busokelo kwenda kujiendeleza kielimu katika chuo hicho na wanabainika kuwa na mtazamo wa kizamani ambao unazingatia zaidi mtaala badala ya ujuzi.

"Wengi unakuta bado wako kwenye ule mfumo wa zamani ambao ni tofauti na ulioelekezwa na serikali, sasa ufundishaji wa mtindo huu unasababisha wanafunzi kutokuwa na ujuzi kama ambavyo mtaala mpya unaelekeza," alisema Dk. Leoncia.

Mwenyekiti wa Chama cha Kuendeleza Masomo ya Hisabati na Sayansi mkoani Mbeya, Zawadi Komba, alisema mfumo wa utunzi wa mitihani unaosimamiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) unazingatia zaidi umahiri wa wanafunzi.

Alisema walimu ndiyo watu wenye wajibu wa kuhakikisha wanafunzi wanakuwa na umahili kwenye kujibu mitihani na kwamba kitendo cha walimu hao kuendelea kutumia mitaala ya zamani ni kupotosha wanafunzi.

Alisema walimu wanatakiwa kupata mafunzo ili wawafundishe wanafunzi kwa kuzingatia mfumo huo mpya ambao unawasaidia kumudu kujibu mitihani.

"Huu mfumo mpya ni mzuri kwa sababu unamuwezesha mwanafunzi kujibu mitihani kwa uelewa na sio wa kukariri kama ilivyokuwa kwenye mtaala wa zamani," alisema Zawadi.

Mwenyekiti wa Chama cha Wakuu wa Shule za Sekondari (TAHOSSA), Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Shaban Mwale, aliwataka walimu wa halmashauri hiyo kuzingatia mitaala mipya inayoandaliwa na serikali ili kuendana na maeneo mengine.

Alisema shule zote za halmashauri hiyo zinatakiwa kuwapima wanafunzi kwa kutunga mitihani inayopima umahili badala ya kupima ufaulu wa zamani.

Akifungua mkutano huo maalumu wa walimu wa masomo ya Hisabati na Sayansi katika Halmashauri ya Busokelo, Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Ernest Hinju, alitoa onyo kwa walimu wanaokiuka mitaala.

Alisema mwalimu yeyote anayekiuka utaratibu huo, atachukuliwa hatua kali za kisheria ili kukomesha utaratibu huo wa walimu wanaokiuka utaratibu wa mitaala ya elimu.




Mustafa Muhammed Ali, akimpima mtoto wake uzito, baada ya kumpeleka katika kliniki ya Hospitali ya Kivunge, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana, utamaduni ambao haujazoeleka kutokana na imani kwamba mama pekee ndiye mwenye jukumu hilo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi: Z'bar ina fursa nyingi za uwekezaji uchumi wa buluu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema Zanzibar ina fursa nyingi za uwekezaji katika sekta ya uchumi wa buluu, kikiwamo kilimo cha mwani na uvuvi wa bahari kuu.

Dk. Mwinyi alitoa kauli hiyo Ikulu Zanzibar alipozungumza na ujumbe wa baadhi ya wawekezaji kutoka Uingereza ulioongozwa na Msaidizi wa Waziri Mkuu katika masuala ya Biashara, Lord Wanley, ambao pia uliambatana na Balozi wa Uingereza nchini, David Concar.

Alisema Serikali anayoiongoza inafurahi kufanya kazi na wawekezaji katika miradi mbalimbali iliyomo katika sekta ya uchumi wa buluu.

Alizitaja baadhi ya changamoto zinazokabili maeneo hayo ni ukosefu wa soko na kiwango kidogo cha bei katika zao la mwani.

Alisema ujio wa ujumbe huo utatoa fursa kwa kampuni mbalimbali zinazohitaji kufanyakazi katika maeneo mbalimbali ya uwekezaji.

Wanley aliwatambulisha baadhi ya wawekezaji alioambatana nao na aina ya miradi ya uwekezaji ambapo miongoni mwa wawekezaji hao ni wanaoshughulika na uwekezaji katika miradi ya kilimo cha mwani, ujenzi wa boti, miundombinu ya barabara na uwanja wa ndege.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, alisema ujio wa ujumbe huo ni hatua ya mwendelezo kutokana na mkutano wa biashara kati ya Tanzania na Uingereza ambao ulifanyika nchini Novemba 16, 2021.

Alisema ujumbe huo umekuja nchini kwa dhamira ya kuangalia fursa za uwekezaji, hususan katika sekta ziliomo katika uchumi wa buluu na maeneo mengineyo.

Alisema ujumbe huo umepanga kukutana na kufanya majadiliano na wafanyabaishara kutoka sekta binafsi katika Hoteli ya Serena Inn.

# Hemed aanika faida za Muungano

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema kuwapo kwa Muungano wa Tanzania kumesababisha kupatikana fursa za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Hemed alitaja fursa hizo katika uzinduzi wa kongamano la miaka 58 ya Muungano wa Tanzania na kumbukumbu ya miaka 50 ya Hayati Sheikh Abeid Amani Karume.

Alisema tangu kuasisiwa kwa Muungano wa Tanzania mwaka 1964, Watanzania wamekuwa wakipata fursa katika nyanja mbalimbali hasa muingiliano wa kidamu na kiuchumi uliopo ambao umesababisha uwapo wa idadi kubwa ya wawekezaji na wafanyabiashara Tanzania.

Alisema Serikali ya Tanzania na Serikali ya Zanzibar zitaendelea kusimamia dhana ya Muungano ili kuuimarisha uzidi kukua kwa maslahi ya watanzania huku akigusia kuondoa kero 11 za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi.

Hemed alieleza uhalali wa Muungano wa Tanzania na kuwataka wananchi kuendelea kuusoma vyema Muungano huo ili kujua historia ya nchi yao.

Alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuitangaza Tanzania katika mataifa mbal mbali, jambo ambalo linakuza diplomasia pamoja kutangaza mengi yaliyopo nchini.

Hemed aliwataka Wazanzibari kuenzi na kulinda jitihada Hayati Karume kwa kushirikiana na wanamapinduzi walijitoa kwa ajili ya Wanzabari na kufanikisha kuasisiwa kwa Muungano wa Tanzania.

Alisema uwapo wa amani na utulivu nchini ni moja kati ya faida kubwa za Muungano ambapo alivipongeza vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuendelea kuhakikisha Tanzania inapiga hatua kiuchumi kwa amani.

Kaimu Waziri wa Nchini Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Harun Ali Suleiman, alieleza kuwa uwepo wa Muungano wa Tanzania ni tunu ya kipekee ambayo ni vyema kuendelea kulindwa.

Akiwasilisha mada kuhusu fursa za Zanzibar katika Muungano wa Tanzania Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk Khalid Salum Muhamed, alieleza kuwa Zanzibar imefaidika katika nyanja mbalimbali katika Muungano akitolea mfano fursa za mikopo, elimu ya juu, pamoja na ulinzi na usalama.

# SMZ yataka uvuvi haramu udhibitiwe

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI za utendaji za wavuvi wa hifadhi ya Kisiwa cha Tumbatu (TUMCA) zimetakiwa kuwa mstari wa mbele katika kupiga vita uvuvi haramu unaoendelea kufanyika katika maeneo ya hifadhi hiyo.

Mkurugenzi wa Idara ya uhifadhi wa maeneo ya Bahari Zanzibar, Dk Makame Omar Makame, aliyasema hayo jana katika kikao cha kujadili maendeleo na changamoto zinazojitokeza katika maeneo ya hifadhi kilichofanyika Maruhubi Mjini Zanzibar.

Dk Makame alisema kutokana na ukaribu uliopo kati ya wavuvi na kamati tendaji ya uvuvi upo uwezekano mkubwa wa kuwatambua wavuvi wanaotumia mitego haramu, hivyo kamati tendaji zinapaswa kutoa taarifa kwa taasisi husika ili kuwadhibiti watu hao .

Aidha alisema Serikali ina mpango wa kuongeza boti mbili kwa ajili ya doria za ukusanyaji wa mapato ya kiingilio cha watalii na doria ya kudhibiti uharibifu unaofanyika katika eneo la hifadhi ya Tumca.

Alisema serikali ya Zanzibar imekuja na sera ya uchumi wa buluu kwa lengo la kuinua uchumi kwa matumizi endelevu kupitia sekta ya ukulima wa mwani, ufugaji wa mazao ya baharini na utalii ambazo ni chachu ya maendeleo.

Naye Meneja wa Hifadhi ya Tumbatu, Said Shaib Said, alisema jitihada za pamoja zinahitajika kwa wakuu wa madiko na maafisa uvuvi pamoja na kamati tendaji za Tumca kusimamia zoezi la wauzaji wa samaki wachanga waliovuliwa kwa uvuvi usiokubalika kisheria ili kupunguza wimbi la uvuvi haramu usizidi kuendelea.

Meneja wa hifadhi ya Ghuba ya Minai, Mwaka Haji Abdalla, aliwataka wavuvi wa dagaa kufuata taratibu za kisheria.

Ofisa Mipango wa Idara ya maeneo ya Hifadhi za Bahari Zanzibar, Mchanga Said Khamis aliwataka washiriki wa kikao hicho kurudi katika shehia zao kutoa elimu waliyopatiwa ya kuachana na uchafuzi wa kimazingira kupitia uvuvi haramu, utumiaji wa taa za kuzamia chini ya bahari na wizi wa samaki katika mahema ya wavuvi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

RAPHAEL EDWARD MCHANI anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA PRIMIO yenye USAJILI NAMBA T418 DWH. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: DAR/STA/RB/155345/2022

## KUPOTEA KWA CHETI



**ZUWENA JUMA MAGAMBO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato che nne chenye index namba **S.1573-0140** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MLANGARINI SEKONDARI** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MOR/MOR/RB/482874/2019.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

AICHI JOSEPH RITALY anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SUZUKI CARRY yenye USAJILI NAMBA T219 DCM, CHASSIS NAMBA DC51T-535039, ENGINE NAMBA F6A6671671. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

TAARIFA POLISI: WMB/RB/314/2022

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na. 678/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU NURDINI MFAUME SAMATA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA KHALIDI NURDINI MFAUME**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2 ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama ya Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 25 Mwezi 4 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 05 Mwezi 04 Mwaka 2022.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda
Wilaya ya Morogoro
Mkoa Wa Morogoro
Usimamizi wa Mirath Na......27....2022
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MUSSA HAMADI MZIRAY WA KIHONDA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA UMMY MUSSA MZIRAY

**TANGAZO**

(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 22/04 /2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia**;
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 19/04/2022

Mwezi 04 Mwaka 2022

## KUPOTEA KWA CHETI



MARY D. LEMA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato che sita chenye index namba S.0332-0653 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MOROGORO SEKONDARI mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/KIL/RB/157278/2022.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SHULE YA MSINGI CHIPOLE -SONGEA MKOANI RUVUMA, inatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina TOYOTA HILUX yenye USAJILI NAMBA T 959 BKH, CHASSIS NAMBA MSP 2L 2446CC. ENGINE NAMBA LN 65 -0071512.Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

POLISI TAARIFA: SO/RB/3219/2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**92 HARDWARE LTD** anatangaza kupotea kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye namba ya USAJILI **T 954 DQL.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

TAARIFA POLISI: **SO/RB/403/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

NASHILA IDDI MTULLA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV 4 yenye namba za usajili T173 BHC. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: SO/RB/400/2022

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT DODOMA**

**MISCELLANEOUS CIVIL APPL. NO. 36 OF 2021**

**DODOMA MUNICIPAL COUNCIL APPELLANT /APPLICANT/PLAINTIFF**

**VERSUS**

**ALLY KAPAYA & 5 OTHERS.................RESPONDENT/DEFENDANT**

**TO: ALLY KAPAYA & 5 OTHERS OF DODOMA**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for/hearing/mention on 02 day of 05, 2022 at 9.00 am. Before **Hon. A.J. MAMBI JUDGE**

**YOUR ARE** required to appear in this Court on the fixed date without fail. And you may bring with you all required documents in support of your case.

Given under my hand and the seal of the court this 25 day of 2,2022

DEPUTY REGISTRAR

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo TEMEKE**
**Ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa wa Dar es salaam**

**Shauri la Madai/Ndoa Na. 536/2022**

**WINFRIDA VALERIAN KIMARO...........Mdai**

**LUHUVILO SIMON SANGA**

**KUITWA SHAURINI**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni na taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: LUHUVILO SIMON SANGA**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 13 mwezi wa 5 mwaka 2022 saa 9:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitolea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20 Mwezi 04 Mwaka 2022.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO**

**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**

**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**

**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB.NA.MMC/69&71/MKUNDI**

**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: MATHEW SEDOYEKA S.L.P 681, MOROGORO**

**ARDHI: KIWANJA NA.69&71 KITALU "P" MKUNDI-MANISPAA YA MOROGORO.**

**MUOMBAJI: METHEW SEDOYEKA S.L.P 181 ,MOROGORO**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa siku 14 toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti

**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana, irudishwe kwa **MKURUGEZI WA MANISPAA -MOROGORO S.L.P 166MOROGORO**

Valency HK
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

PETROAFRICA (T) LTD anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV4 yenye namba ya USAJILI T233 BUV. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

POLISI TAARIFA: SO/RB/401/2022

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**
**KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 77/2019**
**(Asilia Shauri la Uhujumu uchumi Na.1/2018.**
**Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya)**
**JAMHURI.............MRUFANI**
**DHIDI YA**
**KENEDY LUPEMBE SIMSOKWE......MJIBU RUFAA NA.1**
**MATRHEW ELIKANA MWANJALA..........................MJIBU RUFAA NA.2**
**SHABAN MKWICHE................MJIBU RUFAA NA.3**
**KWA BWANA: 1.KENEDY LUPEMBE SIMSOKWE.**
**2.MATHEW ELIKANA MWANJALA**
**3.SHABAN MKWICHE**
**POPOTE MLIPO TANZANIA.**

Mnaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, **Tarehe 25/04/2022** siku ya Jumanne Saa3:00 Asubuhi bila kukosa.

**ELEWENI KWAMBA** Mkikosa kufika siku hiyo Shauri litasikilizwa upande mmoja bila nyinyi kuwepo na Uamuzi kutolewa.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii Tarehe 01/03/2022.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMED S. HASSAN** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba T602 AQR. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**POLISI TAARIFA: SO/RB/399/2022**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Taharuki yaibuka sababu tetemeko, wananchi waomba msaada serikalini

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WANANCHI katika kata ya Ulowa, Halmashauri ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, wamekumbwa na taharuki baada ya kutokea kwa tetemeko la ardhi.

Kutokana na hali hiyo, wananchi hao wameiomba serikali kuwapatia mahema kwa ajili ya kulala nje ili kuepuka maafa yanayoweza kujitokeza.

Baadhi ya wananchi walimwambia mwandishi wa habari hii kwamba kwa sasa wamekuwa na hofu kutokana na tetemeko hilo ambalo limewafanya kuacha kulala ndani ya nyumba hasa kukithiri kwa milipuko mikubwa ambayo imekuwa ikitoka ardhini. Walisema kwa sasa wameamua na familia zao kulala ofisi za kata.

Wananchi hao walitoa kilio chao wakati Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alipotembelea kata hiyo na kujionea taharuki hiyo ambayo imezua hofu kubwa kwa wananchi wa maeneo hayo kwa wakati huu. Walisema milipuko hiyo ilianza tangu Agosti, mwaka jana, na imekuwa ikiongezeka kila siku lakini kwa hiyo ambayo imekuwa kwa sasa imezidi, hivyo wanaomba serikali kufanya uchunguzi na kujua chanzo chake na kuwaondolea hofu waliyo nayo.

Mmoja wa wananchi hao, Donald Shija, alisema milipuko hiyo imekuwa ikitokea hadi mara kumi kwa siku chini ya ardhi mithili ya mabomu na kuongeza kuwa hali hiyo hawajawahi kuona tangu kuzaliwa kwao.

"Nakumbuka mara ya mwisho kusikia tetemeko la ardhi ilikuwa mwaka 1984 na lilikuwa si la namna hii kwani hili limekuwa likilipuka katika eneo moja kwa muda mrefu hali ambayo kwa sisi kama wakazi wa maeneo hayo, tunaomba serikali ifanye uchunguzi kujua chanzo ni nini," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo kuendelea siku hadi siku, wanaomba watafiti wa miamba kutoka serikalini wa kupima eneo hilo kwa kuwa matukio hayo yanatokea mara kwa mara na kuwasababishia hofu wananchi.

Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokaji Wilaya ya Kahama, Mkaguzi Hanafi Mkilindi, aliwataka wananchi kujua kuwa eneo hilo ni mkondo mkubwa na njia ya matetemeko na kuongeza kuwa ni bora wakajenga nyumba imara na zenye lenta lili zisianguke wakati wa milipuko.

Aliwataka wananchi hao wakisikia tetemeko hilo kwenda kujisitiri katika maeneo yaliyo salama kama katika kingo za nyumba, uvunguni au chini ya meza huku walioko nje wasiingie tena ndani ili kuepukana na maafa yanayoweza kutokea.

Naye Kiswaga alisema serikali ina mpango mkubwa wa kutoa elimu ya matetemeko kwa wananchi huku akiongeza kuwa tetemeko hilo si la kawaida na ni la aina yake kwa kuwa limekuwa likitoa milio kama ngoma chini ya ardhi.

Alisema tatizo hilo linaweza kuwa la miamba iliyoko chini kwa kuwa na mgandamizo mkubwa na kuongeza kuwa taarifa za kutokea kwa tukio hilo ni anazo na kuongeza kuwa eneo hilo ni moja ya njia za matetemeko ya ardhi.

Hata hivyo, Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Kimadini wa Kahama, Jeremiah Hango, alisema walifika katika eneo hilo na kusikia mitikisiko na kwamba katika Wizara ya Madini, kuna Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) na wataalamu wake watakuja kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi juu ya hali hiyo.

## Tanzania mwenyeji mkutano PRO Afrika

**Na Maulid Mmbaga**

TANZANIA imepata fursa ya kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa mwaka wa maofisa uhusiano wa umma barani Afrika wenye lengo la kukuza taaluma na ushirikiano wa kisekta.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa Chama cha Wanataaluma wa Uhusiano na Umma nchini (PRST), Ndege Makura, alisema mkutano huo unatarajiwa kufanyika jijini hapo kuanzia Mei 23 hadi 27, mwaka huu na unalengo la kuongeza uelewa kiutendaji na kuimarisha umoja ndani ya Bara la Afrika.

Pia, alisema faida nyingine ya mkutano huo ni kuonyesha dira ya taasisi ya uhusiano wa umma, kutoa fursa ya kuonyesha na kutangaza vivutio vya kiutalii na uwekezaji na kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa kupitia wageni mbalimbali wa kimataifa watakaoshiriki katika mkutano huo.

"Mkutano huo pia utakuwa na matukio matatu ikiwamo kufanya mazungumzo na wanafunzi wa vyuo vikuu wanaosomea uhusiano wa umma na uandishi wa habari kwa ujumla na kukutana na wanataaluma wote wa ndani na nje ya nchi.

"Tukio lingine ni kuwaonyesha fahari zetu kama taifa, kufanya utalii na wageni zaidi ya 300 ambao wamesha idhinisha kuwa watakuja kutoka bara la Afrika, Ulaya na Amerika akiwamo Rais wa Chama cha Maofisa Uhusiano Duniani (IPRA) ya London," alisema Makura.

Aliongeza kuwa huo ni mkutano wa kwanza kufanyika Tanzania ambao pia unatarajiwa kuhudhuriwa na mabalozi wa Afrika wanaowakilisha nchi zao nchini, huku akieleza kuwa huo ni muendelezo wa kampeni iliyoanzia mwaka 2015 ya kusemea bara la Afrika kwa mambo mazuri.

Kwa upande wake Makamu wa Rais wa PRST, Mary Kafyone, alisema chama hicho kiko tayari kushirikiana na serikali katika kulitangaza taifa kupitia mkutano huo na wanaunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kuifungua nchi.

Vile vile, alitoa wito kwa maofisa uhusiano wote nchini kutoka mashirika binafsi na taasisi za umma, kushiriki mkutano huo kwa kuwa watapata fursa ya kujifunza mbinu mbalimbali za jinsi ya kuisemea Tanzania ili izidi kuwa kinara.

"Mara nyingi taarifa za wenzetu zinazotoka kuhusu Afrika na Tanzania zinakuwa hasi, kwahiyo tunataka watu wa uhusiano wa umma (PRO) kubadilisha hiyo dhana na kuhakikisha tunasemea mazuri taasisi zetu na taifa letu ili tuweze kusonga mbele," alisema Mary.




Meneja Uhusiano wa Benki ya CRDB tawi la Premier la Palm Beach, jijini Dar es Salaam, Samia Karim (kulia), akikabidhi pesa taslimu Sh. milioni 10 kwa Mshindi wa bahati nasibu ya Biko, Saida Chitime, mkazi wa Mbagala, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 'Houseboy' mbaroni madai kuua 'housegirl'

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi mkoani Pwani linamshikilia mtu mtu mmoja mwanaume (27) jina limehifadhiwa, kwa tuhuma za kumuua kwa kitu chenye ncha kali mfanyakazi wa ndani, Dawiya Mshihiri(30).

Taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo jana ilieleza kuwa mtuhumiwa ambaye ni mfanyakazi wa kulisha mifugo anadaiwa kufanya tukio hilo Aprili 20 majira ya mchana katika Mtaa wa Mkoani 'B' Wilaya ya Kibaha.

Kamanda Lutumo alisema katika tukio hilo mtuhumiwa alimshambulia Dawiya kwa kitu chenye ncha kali maeneo mbalimbali ya mwili na kumsababishia kifo.

Alisema mtuhumiwa baada ya kutekeleza tukio hilo alijaribu kunywa sumu, lakini hakufanikiwa alikamatwa na kupelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi kwa ajili ya matibabu akiwa chini ya ulinzi.

Kamanda alieleza kuwa chanzo cha tukio hilo kinaendelea kuchunguzwa na wakikamilisha mtuhumiwa atafikishwa mahakamani.

Kamanda Lutumo alisema mtuhumiwa pamoja na marehamu wote walikuwa wafanyakazi katika nyumba ya Samweli.

Mwenyekiti wa mtaa huo, Shabani Kasamia, alisema alipata taarifa ya tukio hilo akiwa Mailimoja ndipo alipopiga simu polisi na kuwajulisha.

Alisema walipofika katika nyumba hiyo wakiwa na polisi walikuta tayari mfanyakazi huyo akiwa ameshafariki akiwa ndani ya nyumba hiyo huku kukiwa na watoto ambao walikua wanashinda na dada huyo.

Alieleza kuwa polisi walipozunguka nyuma ya nyumba kukagua walimkuta kijana huyo akiwa amelala kwenye kitanda nyumba ya uani akiwa amekunywa sumu.

Nipashe ilifika nyumba lilipotokea tukio hilo majirani walielezea kuwa wafanyakazi wote wamekuwa wakifanya kazi katika nyumba hiyo kwa muda mrefu na hawakugundua kama kulikuwa na tatizo kati yao.

# COASTAL UNION YAAHIDI KUANZA KUVUNA POINTI

**Na Cheji Bakari,** TANGA

LICHA ya Coastal Union kuendelea kupata matokeo mabaya katika mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa timu hiyo umesema bado wanayo nafasi ya kujirekebisha na hatimaye kujinusuru kubakia katika ligi hiyo kwenye msimu ujao.

Coastal Union imeendelea kusuasua licha ya kurejea kwa aliyekuwa kocha mkuu, Juma Mgunda ambaye aliwahi kubadilishiwa majukumu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Hamasa ya Coastal Union, Salim Bawaziri aliliambia gazeti hili wanaendelea kujipanga kuhakikisha wanapata matokeo chanya kwenye mechi tisa zilizobakia na amewataka mashabiki na wanachama wao kutokuwa na hofu.

**Bawaziri alisema kupoteza mechi dhidi ya Tanzania Prisons FC ya jijini Mbeya ni hali ya kawaida ya mchezo na wanaamini watafanya vizuri zaidi katika michezo inayofuata.**

"Ile ni hali ya mchezo tu, lakini nataka nikwambie bado tuna nafasi ya kufanya vizuri zaidi," alisema Bawaziri.

Katika mechi tatu ambazo, Joseph Lazaro alikuwa na timu hiyo alishinda moja dhidi ya KMC wakati alipata suluhu dhidi ya Azam FC na kufungwa mchezo mmoja dhidi ya Ruvu Shooting.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Coastal Union ipo katika nafasi ya 13 ikiwa na pointi 21 baada ya kushinda michezo mitano, kutoa suluhu mechi sita na kupoteza michezo tisa.

Katika michezo tisa ambayo Coastal Union imebakiza, mechi nne itacheza nyumbani na iliyobakia watacheza ugenini.

Michezo itakayochezwa nyumbani ni dhidi ya Kagera Sugar, Geita Gold FC, Polisi Tanzania na Biashara United wakati watalazimika kusafiri kuwafuata Namungo FC, Mbeya Kwanza, Mbeya City, Mtibwa Sugar na Dodoma Jiji.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), wakifanya mazoezi kujiandaa mchezo wa marudiano wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia (U-17), dhidi ya Burundi utakaochezwa Mei Mosi, mwaka huu kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar. **PICHA: TFF**

# *Simba Queens, Yanga mawindoni*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma, amesema hatabweteka na ushindi waliopata katika mechi iliyopita ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Ilala Queens na sasa nguvu anazielekeza kuhakikisha pia anawafunga watani zao, Yanga Princess.

Simba Queens ilipata ushindi mnono wa mabao 5-1 dhidi ya Ilala Queens katika mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania uliochezwa kwenye Uwanja wa Mo Arena juzi na kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo.

Mechi kati ya Yanga Princess dhidi ya Simba Queens itachezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Nkoma aliliambia gazeti hili anaendelea kupambana kuhakikisha anashinda mechi zake zote na hatimaye kufikisha malengo ya kutetea ubingwa wanaoushikilia.

"Kuna idadi ya michezo niliyojiwekea katika mbio za kusaka ubingwa na tayari nimeshinda mechi tatu, sasa ni zamu ya kuitazama Yanga Princess, tutahakikisha tunapata pointi tatu muhimu katika mchezo huo," Nkoma alisema.

Kocha huyo alisema anaamini mechi hiyo itakuwa ya ushindani licha ya mchezo wao wa mzunguko wa kwanza kufanikiwa kupata ushindi kwa sababu wapinzani wao wameimarika.

"Malengo yangu ya awali kushinda mechi sita za mwanzo wa mzunguko wa pili, tumefanikiwa kushinda mechi tatu na sasa tunaangalia mechi tatu zijazo, tukianza na pambano letu la Kariakoo Derby dhidi ya Yanga Princess, tumejipanga kuendelea kutafuta pointi tatu," alisema kocha huyo.

Alisema anahitaji kushinda mechi sita zilizobakia ili wafikishe pointi 54 ambazo hazitafikiwa na timu nyingine yoyote inayoshiriki ligi hiyo.

## Nyota sita wa tenisi kuchuana Rwanda

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya vijana ya wenye umri chini ya miaka 12 ya tenisi Afrika yamepangwa kufanyika kuanzia Aprili 26 hadi Mei 2, mwaka huu nchini Rwanda, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Chama cha Tenisi Tanzania (TTTA), Denis Makoi alisema mashindano hayo yatashirikisha nchi wanachama 11 na kwa upande wa Tanzania jumla ya wachezaji sita wanatarajiwa kwenda kupeperusha bendera ya nchi.

Makoi alisema kikosi hicho cha Tanzania kitakuwa na wachezaji wasichana watatu na wavulana watatu, ambao tayari wameshaanza maandalizi kwa ajili ya kushiriki michuano hiyo.

"Lengo la mashindano hayo ni kupata timu ya Taifa itakayoshiriki mashindano ya Afrika ambayo yatafanyika baadaye mwaka huu," alisema Makoi.

Alitaja majina ya wachezaji ambao wataiwakilisha Tanzania katika michuano hiyo ni pamoja na Happy Michael, Nasma Jumanne na Faith Godfrey wakati wavulana ni Hamis Kashimba, Mohamed Hassan na Fredy Ongige.

Aliongeza wachezaji hao wananolewa na makocha wenye uzoefu wa juu katika mchezo huo ambao ni, Majuto Majaliwa na Olais Mollel.

## Geita Gold FC yaikamia KMC

**Na Shufaa Lyimo**

TUMEJIPANGA! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Geita Gold, Felix Minziro kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu.

Minziro aliliambia gazeti hili kikosi chake kiko imara na anaamini hawatazipoteza pointi za mchezo huo.

Alisema anajua wapinzani wao wamejipanga pia, lakini rekodi nzuri waliyonayo Geita inawapa 'jeuri' ya kutamba kuzibakisha pointi nyumbani.

"Tumejipanga vizuri kukutana na KMC , tunajua ni mchezo ambao unatarajiwa kuwa mgumu kwa pande zote, lakini tunasema hawatoboi," alisema Minziro.

Aliongeza tayari ameyafanyia kazi makosa aliyoyabaini katika mchezo uliopita na sasa hivi wachezaji wake wanasubiri muda kutekeleza mafunzo aliyowapatia.

"Lengo ni kupata pointi tatu katika uwanja wetu wa nyumbani, tunazidi kuwaomba mashabiki waendelee kutuunga mkono, tumejipanga kuendelea kuwapa heshima," Minziro alisema.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE SAFI MADRID

REAL Madrid wana uhakika wa kumsajili, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, na watafanya kila wawezalo kumpata mshambuliaji huyo wa Paris St-Germain na Ufaransa baada ya kukubali mlengwa wao mkuu, Erling Braut Haaland, anaelekea Manchester City.(***Mail***)

### BELLINGHAM ATAKIWA

REAL Madrid pia wana nia ya kumleta kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham kule Bernabeu, lakini Borussia Dortmund wanatamani sana kusalia na kinda huyo mwenye umri wa miaka 18. (***Bild***)

### TRAORE ATAKIWA EVERTON

KLABU ya Everton inamfuatilia Adama Traore mwenye umri wa miaka 26 kutoka Wolves kwa nia ya kumsajili winga huyo wa Hispania, ikiwa Barcelona itakataa chaguo la kufanya uhamisho wake wa mkopo Nou Camp kuwa wa kudumu. (***Football Insider***)

### HAG APAEWA BAJETI

KOCHA wa anayekuja wa Manchester United, Erik ten Hag atakuwa na pauni milioni 200 za kutumia kununua wachezaji wapya, huku wachezaji sita wa kikosi cha kwanza wakitarajiwa kuondoka katika msimu wa joto. (***Mirror***)

### MARTIAL KUREJEA

NYOTA Anthony Martial huenda akarejea Old Trafford baada ya kuchezea Sevilla kwa mkopo wa msimu mzima kwa sababu klabu hiyo ya Hispania haijaanzisha mazungumzo ya kusalia na Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 26. (***Fabrizio Romano***)

### POGA HUYO JUVE

WAWAKILISHI wa Paul Pogba wanafanya mazungumzo na Juventus na Real Madrid kuhusu uhamisho wa majira ya joto, wakati kiungo huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 29 atakapokuwa mchezaji huru. (Sky Sports)

### CONTE ATAKA USAJILI

KOCHA wa Tottenham, Antonio Conte yuko tayari kufanya mazungumzo na Daniel Levy kumwambia mwenyekiti wa Spurs kwamba klabu hiyo inahitaji kuwasajili wachezaji sita msimu wa joto, huku kiungo wa kati wa Leicester na Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 24, akiwa kwenye orodha. (***Telegraph***)

### SPENCE ATAKIWA

KLABU ya Tottenham pia inamsaka beki wa kulia wa England, Djed Spence mwenye umri wa miaka 21, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Nottingham Forest kutoka Middlesbrough. (***Mail***)

### KULUSEVSKI KUBAKI

TOTTENHAM itamsajili winga wa Sweden, Dejan Kulusevski kwa mkataba wa kudumu katika majira ya joto. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 yuko kwa mkopo wa miezi 18 na Tottenham wameamua kulipa Juventus ada ya pauni milioni 24.9 msimu huu. (***Evening Standard***)

### CARVALHO ATOA NENO

WINGA wa Ureno, Fabio Carvalho mwenye umri wa miaka 19 amesema nia ya Liverpool ya kutaka kumsajili imeathiri kiwango chake cha mchezo kule Fulham. (***Metro***)

### TONEY ATAKA NYONGEZA

IVAN Toney anataka mkataba mpya na nyongeza ya mshahara kule Brentford, ambako mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 26 yuko chini ya mkataba hadi 2025. (***90 Min***).

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG KOCHA MPYA WA UNITED

## ●●● Afurahia uteuzi huo na kufunguka ni heshima kubwa kwake kupata...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imethibitisha kocha wa Ajax, Erik ten Hag atakuwa kocha wao mpya wa klabu hiyo.

Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 52 amekubali mkataba wa miaka mitatu pale Old Trafford na chaguo la kuongeza mwaka mmoja zaidi na atachukua mikoba kutoka kwa bosi wa muda, Ralf Rangnick, ambaye atahamia katika nafasi ya ushauri.

Akikaribia kutwaa taji la tatu la Eredivisie akiwa na Ajax muhula huu, Ten Hag aliibuka kama chaguo sahihi kwa Mashetani Wekundu katika wiki za hivi karibuni.

Kazi nzuri aliyofanya Amsterdam imemfanya Ten Hag ajijengee sifa kama mmoja wa makocha wanaovutia zaidi katika kandanda duniani na sasa ana jukumu la kurudisha nyakati nzuri kwa mabingwa hao mara 20 wa England.

United kwa sasa wako katika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu England baada ya kichapo cha aibu cha mabao 4-0 kutoka kwa Liverpool Jumanne usiku.

**Ten Hag alisema: "Ni heshima kubwa kuteuliwa kuwa kocha wa Manchester United na nimefurahishwa sana na changamoto iliyo mbele yangu.**

"Naijua historia ya klabu hii kubwa na shauku ya mashabiki, na nimedhamiria kabisa kuendeleza timu yenye uwezo wa kuleta mafanikio yanayostahili.

"Itakuwa vigumu kuondoka Ajax baada ya miaka hii ya ajabu, na ninaweza kuwahakikishia mashabiki wetu kuhusu dhamira yangu kamili na kulenga kukamilisha msimu huu kwa mafanikio kabla sijahamia Manchester United."

Mkurugenzi wa Soka wa United, John Murtough aliongeza: "Katika miaka minne iliyopita akiwa Ajax, Erik amejidhihirisha kuwa mmoja wa makocha wa kusisimua na wenye mafanikio barani Ulaya, anayesifika kwa soka la kuvutia, la kushambulia na kujitolea kwa vijana.

"Katika mazungumzo yetu na Erik kuelekea uteuzi huu, tulivutiwa sana na maono yake ya muda mrefu ya kuirejesha Manchester United katika kiwango tunachotaka kushindana nacho, na ari yake na dhamira yake ya kufikia hilo.


"Tunamtakia Erik kila la heri anapoangazia kufikia mwisho mzuri wa msimu huko Ajax na tunatazamia kumkaribisha Manchester United msimu huu wa joto."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,171,

MECHI KALI
HUDDERSFIELD
VERSUS
BARNSLEY
1 | 1.56
X | 3.86
2 | 5.05

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ARTETA AMSIFU SAKA KWA PENALTI

**LONDON,** England

MIKEL Arteta alimsifu, Bukayo Saka baada ya kuongeza kasi na kufunga penalti yake ya kwanza tangu alipokosa kwenye fainali ya Euro 2020 akiwa na kikosi cha Timu ya Taifa ya England.

Saka mwenye umri wa miaka 20 alifunga penalti hiyo na kumaliza ushindi muhimu wa Arsenal wa mabao 4-2 dhidi ya Chelsea katika dakika za lala salama huku wakimaliza msururu wa vichapo vitatu mfululizo.

Arteta alifichua hakujua ni nani angepiga mkwaju wa penalti baada ya Alexandre Lacazette kutoka nje ya uwanja.

Kocha huyo Mhispania mwenye umri wa miaka 40 alisema: "Nilidhani Gabi (Martinelli) angepiga.

"Nilipoona Bukayo aliichukua, kwa uaminifu, jambo langu la kwanza ambalo nilifikiria lilikuwa nyuma katika msimu wa joto na kile kilichotokea.

"Lakini tena niliwaeleza nyie, hayo yalipotokea Bukayo yalitokea kwa sababu fulani na alijifunza mengi na akakomaa sana ndiyo maana ana msimu ambao amekuwa nao.

"Kwa yeye kuwa na ujasiri wa kusema 'nitaichukua tena' kwa sababu nina hakika ilikuwa nyuma ya akili yake, kwangu ni jambo jema kwake."

Matokeo hayo yanawafanya vijana wa Arteta kusawazisha pointi na wapinzani wao wa London Kaskazini, Tottenham katika vita vya kuwania nafasi ya nne.

Pande zote mbili zimesalia na mechi sita kuchezwa, ikijumuisha mkutano ambao unaweza kuwa muhimu mnamo Mei 12, mwaka huu.

# PSG yakaribia ubingwa Ufaransa

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain ipo kwenye nafasi ya kutwaa taji la Ligi Kuu Ufaransa baada ya mabao ya Kylian Mbappe, Sergio Ramos na Marquinhos kuwapatia ushindi wa magoli 3-0 dhidi ya Angers hapo juzi.

Matokeo hayo yameifanya timu hiyo ya mji mkuu kufikisha pointi 77, ikiiongoza Marseille inayoshika nafasi ya pili, ambayo iliifunga Nantes mabao 3-2, kwa pointi 15 ikiwa imesalia michezo mitano. Iwapo PSG watashinda kwenye Uwanja wa Parc des Princes dhidi ya RC Lens Jumamosi, watatwaa taji hilo.

Stade Rennais wako nafasi ya tatu wakiwa na pointi 56 baada ya kufungwa 2-1 na Strasbourg, ambao sasa wako nafasi ya nne nyuma yao kwa tofauti ya mabao.

Huku Lionel Messi na Marco Verratti wakikosa mchezo huo kutokana na jeraha, PSG walikuwa wenye kiwango bora.

Mbappe aliwaweka mbele kwa bao lake la 22 la ligi msimu huu alipopiga shuti hafifu kutoka nje kidogo ya eneo la hatari ambalo Anthony Mandrea aliweza kugusa kwa ncha ya glavu zake tu.



PSG walimaliza wakiwa na wachezaji 10 baada ya mchezaji wa akiba, Edouard Michut kutolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kumchezea rafu mbaya, Romain Thomas.

## HABARI MICHEZO

# DODOMA JIJI YAFUNGUKA KINACHOWAMALIZA BARA

**Na Adam Fungamwango**

ZIKIWA zimebakia mechi tisa ili kumalizika kwa msimu huu, Katibu Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Fortunatus John amesema uzembe na kutojituma kwa baadhi ya watu katika klabu hiyo ndio kumesababisha kutofanya vizuri kwa timu yao kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.

Dodoma Jiji imekuwa haifanyi vizuri msimu huu tofauti na msimu uliopita, sababu iliyopelekea hivi karibuni kumtimua kocha wake mkuu, Mbwana Makata na nafasi yake kuchukuliwa na Mrundi Masoud Djuma, kocha wa zamani wa Simba. Fortunatus aliliambia gazeti hili sababu nyingine inayowaumiza ni majeruhi ya muda mrefu ya baadhi ya wachezaji wao tegemeo ambao iliwasajili katika malengo ya kukiongezea nguvu kikosi hicho.

"Kuna baadhi ya watu ambao tunadhani hawafanyi kazi yao sawa sawa, hawajitambui kwa nini wapo hapa, hawajui kwa nini wapo Dodoma Jiji, kwa maana hiyo panahitaji msaada ili watu kujitambua na kujitolea," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza hali ya Dodoma Jiji hairidhishi na kwa sasa viongozi wanaendelea kupambana kuhakikisha mambo yanabadilika ikiwamo kuwafanyia semina za kuwaweka vyema kisaikolojia wachezaji wao kwa ajili ya kutimiza vyema majukumu waliyonayo.

"Tuna beki wetu Justin Omari, Augustine Msata na Issa Abushehe, tuliwategemea sana kuibeba timu lakini wote hawa kwa sasa ni majeruhi," Fortunatus alisema.

Hata hivyo, kiongozi huyo amewataka mashabiki wa timu hiyo waendelee kuwa pamoja kwa sababu jitihada za kuhakikisha wanamaliza msimu katika nafasi salama zitafanikiwa.

Dodoma Jiji iko katika nafasi ya 14, ikiwa na pointi 21 baada ya kucheza mechi 20 na imebakiza michezo 10 tu kumaliza msimu.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Asha Jaffari (kulia), akiwania mpira dhidi ya beki wa Ilala Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mo Arena hivi karibuni. Simba Queens ilishinda mabao 5-1. **PICHA: SIMBA SC**

# Mabondia kuzichapa Eid Mosi

**Na Saada Akida**

PAMBANO la kusaka mabondia watakaowasindikiza mchuano kati ya Selemani Kidunda dhidi ya Tshimanga Katompa limepangwa kufanyika siku ya Eid el Fitr kwenye Uwanja wa CCM, Tunduru.

Mratibu wa pambano hilo, Selemani Semunyu alisema lengo la kuandaa mapambano hayo ya utangulizi ni kuendeleza azma yao ya kuhakikisha wanaibua vipaji.

Semunyu alisema maandalizi yanakwenda vizuri na anaamini mchakato huo utawapata mabondia wenye uwezo ambao watapata nafasi ya kutambulisha vipaji vyao.

"Mapambano ya utangulizi kabla ya Kidunda na Katompa yatapatikana kwenye pambano litakalofanyika kwenye sikukuu ya Iddi Mosi, Wilaya ya Tunduru mkoa wa Ruvuma kila kitu kinaenda vizuri na mabondia wanaendelea kujiandaa kwa ajili ya mchezo huo," alisema Semunyu.

Aliwataja mabondia ambao watachuana ni Chidy Benga wa Songea dhidi ya Yazidu Khalfan kutoka Tunduru wakati Kachara Mngama (Tunduru) atazichapa na Junior Junior (Malawi), Julo Julius dhidi ya Mwakinyo Mbabe wote kutoka Tunduru huku Karim Mwenda atachuana na Giliki Giliki (Tunduru), Matula Matula (Tunduru) dhidi ya Aziz Aziz (Songea) na Bashiru Kazembe dhidi ya Kapinga Kapinga wote kutoka Tunduru.

Pambano la Kidunda dhidi ya Katompa ambalo ni la kuwania mkanda wa ubingwa wa WBF litafanyika Julai, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Payback Night ulioko Songea.


,243,460

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/04/22 | 17:00 | Leicester vs Aston Villa | 2.63 | 3.28 | 2.53 |
| 02. 23/04/22 | 17:00 | Hull City vs Reading | 2.48 | 3.17 | 2.77 |
| 03. 23/04/22 | 17:00 | Birmingham vs Millwall | 2.78 | 3.08 | 2.53 |
| 04. 23/04/22 | 17:15 | Fuenlabrada vs Ponferradina | 2.57 | 3.16 | 2.67 |
| 05. 23/04/22 | 20:30 | Adana Demirspor vs Trabzonspor | 2.40 | 3.39 | 2.74 |
| 06. 23/04/22 | 21:00 | Waalwick vs PEC Zwolle | 2.46 | 3.07 | 2.87 |
| 07. 23/04/22 | 21:30 | St. Pauli vs SV Darmstadt | 2.52 | 3.31 | 2.62 |
| 08. 24/04/22 | 16:00 | Burnley vs Wolverhampton | 2.69 | 2.98 | 2.69 |
| 09. 24/04/22 | 16:00 | Bologna vs Udinese | 2.87 | 3.17 | 2.41 |
| 10. 24/04/22 | 16:00 | Metz vs Brest | 2.98 | 3.22 | 2.33 |
| 11. 24/04/22 | 17:15 | UD Ibiza Eivissa vs Las Palmas UD | 2.79 | 3.13 | 2.49 |
| 12. 24/04/22 | 18:30 | Hertha BSC vs Stuttgart | 2.73 | 3.22 | 2.48 |
| 13. 24/04/22 | 21:45 | Lazio vs AC Milan | 2.78 | 3.27 | 2.41 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA

"X" - NI TIMU KUTOKA SARE

"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 22/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5665 | Jeonbuk Hyundai vs Hoang Anh Gia Lai | 1.52 | 3.89 | 5.45 |
| 16:00 | 1023 | Gorilla FC vs Gasogi United | 2.37 | 2.78 | 3.13 |
| 16:00 | 2706 | Mbeya Kwanza FC vs Coastal Union | 2.49 | 2.68 | 3.07 |
| 16:00 | 3546 | Etoile de Lest vs Bugesera FC | 2.95 | 2.81 | 2.47 |
| 16:00 | 5442 | Espoir FC vs Rutsiro FC | 2.83 | 2.78 | 2.59 |
| 17:00 | 1794 | Rabotnicki Sk vs FK Skopje | 1.58 | 3.40 | 5.83 |
| 17:00 | 2555 | Sydney FC vs Yokohama F Marinos | 5.27 | 4.10 | 1.50 |
| 17:00 | 2622 | Terengganu vs Selangor FC | 2.19 | 3.40 | 2.87 |
| 17:00 | 3559 | Vissel Kobe vs Chiangrai Utd | 1.49 | 3.99 | 5.64 |
| 17:00 | 5465 | Astana vs FK Kaspiy Aktau | 1.46 | 3.73 | 6.78 |
| 17:45 | 5210 | Ol. Medea vs RC Relizane | 1.39 | 3.80 | 8.38 |
| 18:00 | 1653 | Zalgiris Kaunas vs Vilniaus Riteriai | 2.53 | 3.22 | 2.53 |
| 18:00 | 3643 | Lahti vs KuPS Kuopio | 5.07 | 3.71 | 1.58 |
| 18:00 | 3715 | FC Balti vs Dinamo-Auto | 2.04 | 3.65 | 2.97 |
| 18:00 | 3940 | Haka vs Hifk | 1.63 | 3.45 | 5.05 |
| 18:00 | 5669 | Neman Grodno vs Shakhter Soligorsk | 4.38 | 3.26 | 1.77 |
| 19:00 | 1265 | Levski Sofia vs Ludogorets Razgrad | 2.78 | 3.31 | 2.28 |
| 19:00 | 1403 | Tallinna Kalev vs Tammeka Tartu | 6.22 | 4.66 | 1.38 |
| 19:00 | 5927 | Radomiak Radom vs Cracovia | 2.24 | 3.01 | 3.11 |
| 19:30 | 1161 | Fortuna Dusseldorf vs Dynamo Dresden | 1.70 | 3.66 | 4.55 |
| 19:30 | 2579 | Karlsruher SC vs Ingolstadt | 1.86 | 3.61 | 3.76 |
| 20:00 | 1836 | Gaz Metan Medias vs Dinamo Bucuresti | 23.71 | 8.50 | 1.09 |
| 20:00 | 4954 | Sonderjyske vs Vejle BK | 2.23 | 3.37 | 3.03 |
| 20:15 | 1059 | Sepahan Esfahan vs Pakhtakor | 2.12 | 2.87 | 3.56 |
| 20:15 | 2818 | Shabab AL Ahli Dubai Club vs Ahal FC | 1.40 | 4.37 | 6.41 |
| 20:15 | 3073 | Quwa Al Jawiya vs Jazira Abu Dhabi | 2.69 | 2.93 | 2.59 |
| 20:30 | 2044 | Caykur Rizespor vs Fenerbahce | 4.59 | 3.89 | 1.67 |
| 20:30 | 3739 | FC Schaffhausen vs FC Wil | 1.83 | 3.69 | 3.55 |
| 21:00 | 1608 | Twente vs Sparta Rotterdam | 1.59 | 3.92 | 5.15 |
| 21:00 | 3532 | Ittihad Kalba vs Al Nasr Dubai | 2.58 | 3.31 | 2.44 |
| 21:00 | 3635 | MTK Budapest vs Mezokovesdi SE | 2.23 | 3.25 | 2.91 |
| 21:15 | 1134 | FC Vaduz vs Neuchatel Xamax | 1.92 | 3.45 | 3.45 |
| 21:30 | 1713 | VfL Wolfsburg vs Mainz | 2.46 | 3.18 | 2.79 |
| 21:30 | 4809 | Zaglebie Lubin vs Gornik Zabrze | 2.63 | 3.16 | 2.48 |
| 21:30 | 5849 | LKS Lodz Pss vs Chrobry Glogow | 1.73 | 3.46 | 4.28 |
| 21:45 | 1017 | Bohemians FC vs Shamrock Rovers | 3.59 | 3.21 | 1.96 |
| 21:45 | 1138 | Huddersfield vs Barnsley | 1.56 | 3.86 | 5.54 |
| 21:45 | 3129 | Wexford Youths vs Waterford Utd | 3.90 | 3.70 | 1.74 |
| 21:45 | 3142 | St Patricks vs Finn Harps | 1.59 | 3.64 | 5.05 |
| 21:45 | 3712 | Kilmarnock vs Arbroath | 2.02 | 3.20 | 3.60 |
| 21:45 | 5564 | Derry City vs UCD Dublin | 1.18 | 5.84 | 12.65 |
| 21:45 | 5816 | Dundalk FC vs Shelbourne | 1.73 | 3.40 | 4.38 |
| 21:45 | 5832 | Galway United vs Bray Wanderers | 1.60 | 3.71 | 4.88 |
| 21:45 | 5908 | Cobh Ramblers vs Cork City | 8.73 | 4.75 | 1.29 |
| 22:00 | 1640 | Tenerife vs Huesca | 2.04 | 3.12 | 3.71 |
| 22:15 | 1289 | FC Vizela vs FC Arouca | 2.14 | 3.29 | 3.29 |
| 23:15 | 1337 | Al Gharafa SC vs Foolad Khuzestan | 4.09 | 3.26 | 1.82 |
| 23:15 | 2104 | Al Shabab Riyadh vs Mumbai City FC | 1.16 | 6.25 | 12.69 |
| 23:15 | 5795 | Al Taawon vs Lekhwiya SC | 3.16 | 3.50 | 2.01 |
| 23:30 | 5032 | Ayacucho vs Atletico Grau | 1.59 | 3.64 | 5.05 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Ijumaa Aprili 22, 2022

Nipashe



## Ten Hag kocha mpya wa United

UKURASA 21

AMEREJEA...



Nahodha wa Simba, John Bocco akifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji Orlando Pirates itakayochezwa Jumapili nchini Afrika Kusini. Bocco hakucheza mechi iliyopita kutokana na kutumikia adhabu ya kadi tatu za njano. **PICHA: SIMBA SC**

# Yanga yaiongezea dozi Namungo FC

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi akitamba kikosi chake kiko tayari kusaka ushindi katika kila mechi watakayocheza ili kufikia malengo, tayari viongozi wa klabu hiyo wameingia msituni kusajili nyota wapya watakaoitumikia timu hiyo kwenye msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki, imeelezwa.

Tayari Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili, Hersi Said ameanza mchakato wa kufuatilia ligi za nchi jirani kwa ajili ya kuangalia wachezaji baada ya Nabi kutoa agizo la kuhitaji mshambuliaji pamoja na nyota, Stephane Aziz Ki wa Asec Mimosas.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema wamejipanga kufanya usajili mkubwa kwa sababu msimu ujao watashiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Bumbuli alisema muda ukifika wataweka wazi kila kitu ikiwamo hatua ya mazungumzo ambayo wamefikia na Aziz Ki pamoja na nyota wengine wanaotakiwa na kocha wao (Nabi).

"Muda wa usajili bado, kuhusu Aziz Ki ni mchezaji mzuri lakini suala la kumalizana na Yanga hilo bado, ukifika muda wa usajili basi halitafichika," alisema Bumbuli.

Aliongeza kwa sasa akili na nguvu zao wanazielekeza katika mchezo wao dhidi ya Namungo FC na anaamini watapata matokeo mazuri na kuendelea na kampeni zao za kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Ni jambo la furaha kurejea kwa baadhi ya wachezaji wetu waliokua majeruhi lakini, tunatakiwa kuwaheshimu wapinzani kwa sababu wamekuwa na safu imara ya ushambuliaji na kupata matokeo mazuri katika michezo yao ya hivi karibuni," alisema Nabi.

Naye Meneja wa Namungo FC, Steven Josiah aliliambia gazeti hili kwa sasa kikosi chao kipo katika mazoezi makali kwa ajili ya kuhakikisha wanapata ushindi kwenye mechi hiyo.

"Nguvu kubwa tunayoiweka kwa sasa ni kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika mechi inayokuja. Kama mechi nyingine huwa tunapata matokeo mazuri kwa nini isiwe kwa Yanga? Kwa nini ushindi ukosekane? Itakuwa mechi nzuri, na tunaamini itakuwa moja kati ya mechi bora sana msimu huu," alisema Josiah.

# Simba yaimarisha ulinzi

## ●●● Kambini Dar hadi Sauzi itakapofikia, yapaa na ujumbe mzito...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikijiandaa na safari ya kuelekea Afrika Kusini kuwafuata Orlando Pitares kwa ajili ya mechi ya mkondo wa pili ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, hali ya ulinzi katika kikosi cha Simba imeimarishwa ili kuepukana na vitendo vya hujuma, imefahamika.

Orlando Pirates itaikaribisha Simba katika mchezo huo wa marudiano utakaochezwa keshokutwa mjini Soweto.

Kikosi cha Simba, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na wawakilishi pekee wa nchi waliobakia katika mashindano ya kimataifa walitarajiwa kuondoka nchini jana au leo kuelekea Afrika Kusini kukamilisha dakika 90 zilizobakia.

Hata hivyo, taarifa zilizopatikana kutoka katika kambi ya Simba iliyopo Mbweni, Dar es Salaam, inasema wachezaji wa timu hiyo wameongezewa ulinzi zaidi tofauti na ule wa awali uliozoeleka.

Chanzo hicho kinadai ulinzi uliowekwa kambini hautokani na kujilinda na maneno ya Kocha, Mandla Ncikazi aliyoyatoa baada ya mechi ya Jumapili iliyopita, la hasha, ila ni kuzuia utoro wa baadhi ya wachezaji pamoja na hofu ya kuwepo hujuma.

Chanzo hicho kilisema viongozi wa Simba wameonekana 'kupania' na wamejipanga kuona timu hiyo inafuzu hatua ya nusu fainali na kwa sababu hiyo, hawataki masihara licha ya kuwawekea bonasi nzito.

Taarifa zaidi zinasema mabosi wa timu hiyo wamechukua hatua zote zinazostahili za maandalizi lakini pia wanahakikisha wanazuia kila kitu ambacho kitaonekana kinaweza kuharibu mipango ya ushindi waliyoiweka.

Simba iliingia kambini Jumanne ikiwa ni siku mbili baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 katika mechi ya kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini na hivyo kuhitaji sare au ushindi wa aina yoyote ili kusonga mbele katika michuano hiyo ya kimataifa.

Chanzo hicho kiliongeza Simba kupitia ofisi ya ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini imeomba kupatiwa ulinzi imara baada ya timu hiyo kuwasili ugenini kwa ajili ya mechi hiyo ya marudiano hadi itakapomaliza majukumu yake na kurejea nyumbani.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili jana wameamua kufanya hivyo ili wasipate bugudha yoyote hasa kufuatia maneno yaliyotolewa na wenyeji wao ambayo yanaweza kuchochea hisia.

"Tumetoa taarifa kwenye mamlaka za huko, pamoja na ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini ili kupatiwa ulinzi wa kutosha na wa uhakika, tukitua kwenye Uwanja wa Ndege ya Oliver Tambo kusiwe na bugudha, lakini maisha yetu ndani ya Sauzi yasiwe na shida, ukirejea maneno ya uchochezi ya kocha wa Orlando Pirates aliyoyatoa," Ahmed alisema.

Meneja huyo alisema tayari baadhi ya watu wameshatangulia kuweka mambo sawa, huku nahodha wa timu hiyo, John Bocco akiwa amesharejea kikosini lakini pia, Joash Onyango na Sadio Kanoute nao wamerudi kufuatia kukosekana katika mechi iliyopita kwa sababu ya kutumikia adhabu ya kadi tatu za njano.

"Natamani siku moja wasemaji watatu tunakua busy na CAF, sio kama sasa hivi niko peke yangu, nakua kama ninawaonea Zaka Zakazi (Msemaji wa Azam FC) na Hassan Bumbuli (Yanga), halafu wananionea wivu,... tukifanikiwa kufika nusu fainali tutapita na Jangwani, tutaimba na kucheza halafu tuwakumbushe historia wanayojivunia haitawasaidia popote," alitamba msemaji huyo wa Simba.

Kabla ya mechi dhidi ya Orlando Pirates, Ahmed aliongoza mashabiki kuzunguka sehemu mbalimbali jijini kwa ajili ya kuhamasisha kujitokeza uwanjani kushuhudia mchezo huo muhimu ambao walipata ushindi.

9 770856 541002